SUPA JACKPOT
TZS. 1,087,305,640
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 19

**MIAKA 2 YA SAMIA**
Wadau wasema dhamira yake yaonekana zaidi kwa matendo



KINAMAMA WANAPOJIVUNIA WIKI YAO... SIDO Moro yang'ara nao, ikionyesha kundi njia, hata wakasimama na miradi uchumi (Ukurasa 12)

Hoja ya Lema kuhusu bodaboda isigeuke kuwa malumbano kisiasa (Ukurasa 13)

BUFE
IJUMAA MACHI 10, 2023
Nipashe

JOTO WIKI WANAWAKE.., Lilian Kawa; 'jembe' la benki kutwaa tuzo za umahiri Afrika (Ukurasa 14)

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA...
Ziara zake 'zajibu', wawekezaji 270 wa EU waja nchini kujadili biashara, miradi
• Waingia mikataba zaidi Sh. trilioni moja
• Benki iliyoondoka miaka 16, yarejea

Hashil Abdallah, anaueleza mkusanyiko huo wa siku mbili, kwamba ni matokeo ya ziara yake Rais Dk. Samia alizofanya katika nchi za EU, kwa lengo la kuifungua Tanzania katika uchumi wa dunia.

Makamu wa Rais wa Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB), Thomas Ostros, akaweka wazi sababu za kurejea Tanzania baada ya kutokuwapo kwa miaka saba, ni kuridhishwa na maboresho ya mazingira mazuri ya biashara yaliyofanywa na Rais Samia.

Pia, bosi huyo wa EIB, akataja sababu nyingine ya kurudi nchini ni baada ya UVIKO-19 kufifia nchini, hapo nyuma ya pazia kukionekana juhudi za Rais Dk. Samia.

na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, pia Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht.

Lengo lake ni kuongeza safari za ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Kisiwa cha Mayotte, Ufaransa, ifikapo mwezi Juni, mwaka huu.

Mikataba mingine ni kati ya Bandari ya Antwerp-Bruges International na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania, itakayoongeza usimamizi na kuimarisha miundombinu, ikiwamo bandari kavu na za maziwani, kuziongezea uwezo na ufanisi.

Pia, kukawapo hati ya makubaliano zinazohusu ujenzi wa Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Kakono Hydro Power, mkoani Kagera uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika...

KILICHOJIRI MKUTANONI

UKURASA 11

# Nipashe
Ijumaa Machi 10, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
MWANGA WA JAMII
ISSN 0856 • Na. 0581245
www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

## MJUMBE BODI YA CHADEMA:
# Sishangai kina Mdee kutoondolewa bungeni



UKURASA 2



Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, SACP Wilbroad Mutafungwa, akitoa heshima za mwisho kwenye jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mwandishi na Mwakilishi wa gazeti la Nipashe Kanda ya Ziwa, marehemu Richard Makore, wakati wa kuagwa jijini Mwanza jana, kabla ya kusafirishwa kwenda nyumbani kwao Kijiji cha Remng'orori wilayani Serengeti mkoani Mara kwa maziko. Wa pili kushoto ni Mhariri Mtendaji Msaidizi wa gazeti la Nipashe, Epson Luhwago. **PICHA: VITUS AUDAX**

# RPC aongoza kuaga mwili wa mwandishi wa Nipashe

UKURASA 3

# Mawaziri kikaangoni kwa Katibu Mkuu CCM

UKURASA 5

**MICHEZO** NABI AFICHUA SIRI YA USHINDI YANGA UK. 24

**KATUNI** UK. 6



Mkurugenzi Mtendaji wa Tanzania LPG Association, Amos Mwansumbue, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maonyesho ya gesi ya kupikia ya Afrika Mashariki 2023 (LPG Expo) yanayotarajiwa kufanyika tarehe 15 hadi 16 mwezi huu kwenye hoteli ya Rotana. Kulia ni Mkurugenzi Mkuu wa LPG Expo ambao ndio waandaaji wa maonyesho hayo, Catherine Ho. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mjumbe Bodi CHADEMA: Sishangai kuona kina Mdee wakiwa bungeni

**Na Kulwa Mzee**

MJUMBE wa Baraza la Wadhamini CHADEMA, Dk. Azaveli Lwaitama, amedai mahakamani kuwa wabunge wa Viti Maalum, Halima Mdee na wenzake 18 walitamkwa kuitwa wabunge na mamlaka yenye shaka.

Pia amesema hashangai kuwaona wanasiasa hao 19 wakiwa bungeni kutokana na alichokiita ukakasi wa kiutawala wakati wa serikali iliyopita.

Mjumbe huyo alitoa kauli hiyo jana alipohojiwa kizimbani kwa takribani saa tatu huku akilalamikia maswali ya mtego ya wakili alisisitiza avumiliwe kwa majibu yake.

Dk. Lwaitama alidai hayo Mahakama Kuu, Masjala Kuu Dar es Salaam mbele ya Jaji Cyprian Mkeha katika shauri la kupinga kuvuliwa uanachama lililofunguliwa na Mbunge Halima Mdee na wenzake 18 dhidi ya CHADEMA, Tume ya Taifa ya Uchaguzi na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

"Waliapishwa kuitwa wabunge kwa sababu utaratibu haukufuatwa, ilikuwa taharuki, watu wanashangaa, ilikuwa wakati wa Magufuli haikushangaza sana.

"Walitamkwa kuwa ni wabunge. Nchi hii wakati wa Magufuli unaweza kutangazwa mbunge hata haujachaguliwa. Mamlaka hizo zilikengeuka wakati huo.

"Kutangazwa na mamlaka yenye shaka, hilo ni jambo lingine, siwezi kukubaliana na vitu vilivyokuwa vinafanywa wakati wa Magufuli," alidai Dk. Lwaitama wakati anajibu maswali ya Wakili wa wabunge hao, Ipilinga Panya.

Alidai kuwa kipindi cha uongozi wa Magufuli, ilifika mahali kichwani unashindwa kuelewa kwa kuwa mamlaka zilikengeuka.

"Mimi ninajibu navyofikiria mimi, mawakili ninaomba uvumilivu. Uteuzi wa wabunge wa viti maalum katika mazingira ya kawaida, lakini sio hayo ya mwaka 2020. Tume (NEC) ndio inatoa majina kwa spika na tume inapokea majina kutoka kwenye chama.

"Chama kikiwa hakikutaki, ondoka! Unang'ang'ania nini? Mtu huruhusiwi kuwa bungeni, unakuwa bungeni! Ninaiheshimu Katiba ndio maana ninashangaa watu wanakuwa bungeni wakati sio wanachama (wa chama cha siasa)," alidai Dk. Lwaitama.

Alidai alijiunga na CHADEMA mwaka 2015 kama mwanachama hadi alipoombwa kuwa Mjumbe wa Bodi ya Wadhamini Novemba 2022.

Dk. Lwaitama alidai kila mahali kuna utaratibu wa nidhamu, inategemea makubaliano ya kikundi chenyewe katika kumwajibisha mtu akikiuka makubaliano.

Alidai kama kikundi cha hiari, mkikubaliana ukaona makubaliano yanakubana, unaacha kwani hata yeye akiona wanafanya mambo hayafanani na yeye, saa yoyote anaweza kujiondoa kama watamwekea masharti ya kumbana.

"Usipofuata utaratibu wanakutenga kwenye kikundi, mamlaka ndio inatamka fulani, siku fulani hakufuata utaratibu, miiko na kanuni. Ukijiunga kwenye kikundi, kikisema unakiuka utaratibu jiondoe kwani lazima, kwani ni uraia?" alihoji.

Dk. Lwaitama alidai alishauriwa na Mwanasheria wa CHADEMA kuapa kiapo kinzani kilichojibu kiapo cha waleta maombi.

"Mheshimiwa Jaji, huyu Mheshimiwa mwanafunzi wangu naye... sina wasiwasi na kiapo ninachoulizwa maswali.

"Kwa taarifa iliyotolewa, wabunge 19 walishafukuzwa, mamlaka ilikuwa haijapeleka majina huko wanakoteuliwa, na walikubaliana wasipeleke, waliibukia huko, aliyekuwa gerezani akaibukia huko, ikawa taharuki, nilikuwa Bukoba," alidai.

Katika shauri hilo, CHADEMA inawakilishwa na Wakili Peter Kibatala. Upande wa mjibu maombi namba mbili, NEC na namba tatu Mwanashweria Mkuu wa Serikali, unawakilishwa na Wakili Stanley Kalokola na Wakili Kausa Kilonzo. Waleta maombi, Mdee na wenzake 18 wanawakilishwa na Wakili Ipilinga Panya, Aliko Mwamanenge, Edson Kilatu, Humphrey Malenga na Joyce Mwakapila.

Mahakama imetoa kibali kwa upande wa serikali kuhoji wajumbe wa Bodi ya Wadhamini CHADEMA katika hoja za kisheria. Shauri linatarajiwa kuendelea leo, Dk. Lwaitama anaendelea kuhojiwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
10.03.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Jumamosi** tarehe **11-03-2023** kampuni ya **Spedag Interfreight Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar- Es- Salaam Port kuelekea Mzenga,** gari hiyo ina namba ya usajili: **NRB 69149 / NRB 4343293**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   - **Urefu - mita 36.00**
   - **Upana - mita 6.60**
   - **Kimo - mita 4.60**

3. Njia itakayotumika: **Bandari ya Dar-Es-Salaam hadi Mzenga** kupitia **Morogoro Road** Gari itasafiri muda wa usiku ***(Kuanzia saa 08:00 Usiku mpaka saa 11:00 Alfajiri)*** Kutoka **Dar- Es- Salaam Port mpaka Mlandizi Kutoka Mlandizi kwenda Mzenga** gari itasafiri muda wa mchana ***( kuanzia 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

## Zitto: Tuache siasa za kutishana, tuwe na hoja

**Na Julieth Mkireri,** RUFIJI

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema chama hicho kinataka maridhiano ambayo yanazungumzwa kitaifa yashuke chini ili kuboresha mazingira ya kufanya siasa.

Amesema kuna haja kuwapo mabadiliko kwa kuacha mazingira ya siasa za kutishana badala yake kuwe na siasa za hoja na kujikita kwenye namna ya kutatua kero za wananchi.

Zitto aliyasema hayo jana alipohutubia wananchi wa Ikwiriri, Wilaya ya Rufiji mkoani Pwani katika mwendelezo wa mikutano yao kisisa, akisisitiza kuwa serikali inatakiwa kuondoa utawala wa viongozi wa kijeshi na vyombo vya usalama ili kufanyika siasa zisizo na hofu kwa wananchi.

Alisema wanasiasa wanatakiwa kufanya siasa za maridhiano ambazo watakuwa wakishirikiana vizuri na wananchi badala ya kutishana kwa sababu zisizo na tija.

Awali akizungumza na wananchi eneo la Mwandege na Vikindu wilayani Mkuranga, Zitto alimshukuru Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Khadija Nasri na viongozi wengine kwa kujitokeza kuwapokea viongozi wa chama hicho.

Zitto alimwomba mkuu wa wilaya huyo aliyefuatana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Mwantumu Mgonja, kuendelea kutoa ushirikiano kwa vyama vingine vya siasa kama anavyofanya Rais Samia Suluhu Hassan. Kiongozi huyo pia alimtaka mkuu wa wilaya kutenda haki kwa makundi mbalimbali wakiwamo vijana na wafanyabiashara katika shughuli zao.

Pia aliwataka wananchi na vyombo vya usalama kuwatumia mawaziri vivuli wa mambo ya ndani na wengine wa chama hicho kutoa kero zao ili wazisemee na kupatiwa ufumbuzi.

Mkuu wa Wilaya hiyo, Khadija, alisema kuwapokea viongozi wa chama hicho ni utaratibu walioujiwekea wilayani mwake.

"Leo (jana) tulipopata taarifa ya ujio wa viongozi wa ACT-Wazalendo, tukaona sisi viongozi wa serikali ni jukumu letu. Usalama wao pale wanapokuwa wilaya ya Mkuranga ni jukumu langu kuhakikisha wananchi wanaoingia mpaka wanatoka wanatakiwa kuwa salama, ninatimiza jukumu langu la msingi," alisema.

Msemaji wa Mambo ya Ndani wa chama hicho, Mbarala Maharagande, alisema serikali inatakiwa kuona umuhimu wa kuanza kuwalipa fidia wananchi walioathirika na matukio ya kimabavu na ukiukwaji wa haki za binadamu.

Katika ziara hiyo Zitto amefuatana na Mwenyekiti wa chama, Juma Duni Haji, Katibu Mkuu, Ado Shaibu na mawaziri kivuli wa sekta mbalimbali.

## HABARI KITAIFA




Mkuu wa Ukaguzi wa Mahesabu wa Ndani wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Joyce Maduhu (wa pili kulia), akikabidhi vitu mbalimbali kwa Muuguzi Kiongozi wa Taasisi ya Saratani ya Ocean Road (ORCI), Chausiku Chapuchapu, vilivyotolewa msaada na benki hiyo, hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam juzi, kwa ajili ya wagonjwa wa saratani ikiwa ni sehemu ya kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RPC aongoza kuaga mwili wa mwandishi wa Nipashe

**Na Pendo Thomas,** MWANZA

MWILI wa Mwandishi Mwandamizi wa Gazeti la Nipashe Mkoa wa Mwanza, Richard Makore, aliyefariki dunia Machi 7, mwaka huu, kwa ajali ya basi mkoani Geita, umeagwa nyumbani kwake Mtaa wa Lumala, Manispaa ya Ilemela.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Wilbroad Mutafungwa, jana aliongoza waombolezaji kuaga mwili wa Makore na baadaye kufuatiwa na ibada kisha mwili kusafirishwa kwenda Kijiji cha Remng'oroli wilayani Serengeti mkoani Mara kwa ajili ya maziko.

Akitoa salamu za rambirambi, Kamanda Mutafungwa alisema alipokea kwa mshtuko taarifa za kifo cha mwandishi huyo kilichosababishwa na ajali, akisisitiza jamii kuendelea kufuata sheria na taratibu za matumizi ya barabara ili kuepukana na vifo vya aina hiyo. Kamanda huyo aliwahi kuwa Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani nchini kabla ya kuhamishiwa mkoani Mwanza kuwa Kamanda wa Polisi wa Mkoa.

Mwakilishi wa Kampuni za IPP Media, Epson Luhwago alisema Kampuni ya The Guardian Limited inayomiliki Gazeti la Nipashe alilokuwa anafanyia kazi Makore na tasnia ya habari kwa ujumla wamepoteza mtu muhimu aliyekuwa mstari wa mbele kutumia kalamu yake kusaidia jamii bila kuogopa.

"Tulipopata taarifa hizi zilitushtua sana, hatukuamini hadi siku iliyofuata asubuhi tulipopata uhakika. Kwa kweli ilibidi tukubali lakini inaumiza sana," alisema.

Luhwago alimwelezea Makore kama mtu mpenda haki na msema kweli katika utendaji wake, na alama hiyo itabaki mioyoni mwa wanatasnia ya habari kama kumbukumbu ya kuenzi mazuri aliyoyafanya enzi za uhai wake.

Alisema Kampuni ya The Guardian Limited itaendelea kuwa bega kwa bega na familia ya marehemu katika mambo muhimu hadi kukamilisha utaratibu wa kumhifadhi Makore kwenye nyumba yake ya milele. Meneja wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Kanda ya Ziwa, Fransis Mihayo, alisema alimfahamu Makore kupitia ufuatiliaji wake wa kazi za habari na kwa kipindi chote alikuwa mtu anayejituma, hivyo baada ya kupokea taarifa za msiba huo wameamua kuungana na familia ya wanahabari kuomboleza kifo chake.

Makore aliyefariki dunia katika ajali ya basi la Kampuni la Sheraton lililokuwa likitoka mkoani Mwanza kuelekea Geita, ameacha mke na watoto wawili wa kike na wa kiume.

# Hospitali yapima figo bila malipo

**Na Joseph Mwendapole**

HOSPITALI ya Regency ya jijini Dar es Salaam imeandesha kambi ya kupima bure magonjwa ya figo ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Figo Duniani inayofanyika Machi 9 kila mwaka.

Kambi hiyo ya upimaji figo ilifanyika jana kwenye Zahanati ya Regency iliyoko Mtaa wa Zanaki katikati ya Jiji, ambako wataalamu wa figo watatoa ushauri wa bure kwa watakaofika.

Akizungumza na Nipashe jana, Daktari Bingwa wa Hospitali hiyo, Sudakshnina Ghosh alisema kambi hiyo ya upimaji na ushauri kuhusu maradhi ya figo hufanywa kila wiki ya pili ya mwezi wa tatu kila mwaka.

Alisema kwenye kambi hiyo, wananchi walipimwa kisukari, shinikizo la damu, uzito, mkojo, urefu ili kubaini watu wenye matatizo ya figo na kuwapa ushauri wa kitaalamu.

"Kwa siku nzima leo (jana) tutapima maradhi ya figo na kisha utatolewa ushauri wa kitaalamu kwa wale watakaoonekana wana dalili ya matatizo ya figo, wataalamu wa lishe nao wapo kutoa ushauri kuhusu namna bora ya kula kwa sababu chakula kina mchango mkubwa katika kuzuia maradhi ya figo," alisema.

Dk. Ghosh alisema watu wanaweza kuishi vizuri na maradhi ya figo kama watayatambua mapema na kwamba kwenye kambi hiyo watawaelimisha watu kuhusu tatizo hilo ambalo linazidi kuongezeka duniani.

Alisema kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), inakadiriwa mtu mmoja kati ya watu 10 ana maradhi ya figo na wale wenye miaka 65 na kuendelea mtu mmoja kati ya watano ana matatizo ya figo, hali ambayo alisema inazidi kuwa mbaya.

Alisema kwenye kambi hiyo watawapa elimu wananchi kuhusu kuongezeka kwa maradhi ya figo hivyo kuwa na ulazima wa kupima afya mara kwa mara kabla hali haijawa mbaya.

Alisema mara nyingi ugonjwa wa figo huwa hauonyeshi dalili zozote, hivyo mgonjwa anapoamua kwenda hospitalini anakuwa amechelewa na ugonjwa huo kufikia asilimia 90 na kuhitaji matibabu ya muda mrefu au upandikizaji wa figo mpya.

"Gharama ya upandikizaji wa figo ni kubwa sana. Kwa hiyo, njia pekee nafuu ya kuzuia maradhi hayo ni kupima mara kwa mara kujua afya ya figo yako.

"Ni nani wanaweza kupata maradhi ya figo? Mtu yeyote wa rika lolote, rangi yoyote na umri wowote anaweza kupata huu ugonjwa lakini walioko hatarini zaidi ni wale wenye kisukari, shinikizo la damu, watumiaji wa dawa za kupunguza maumivu kwa muda mrefu, watumiaji wa sigara na walevi wa kupindukia," alisema.

Alisema njia bora ambayo watu wanaweza kuepukana na maradhi hayo ni kujenga utamaduni wa kupima mara kwa mara afya ya figo hasa wenye umri kuanzia miaka 35 na kuendelea.

Daktari bingwa huyo alisema yalikuwa maono ya mwanzilishi wa hospitali hiyo, Hayati Dk. Rajni Kanabar kwamba hospitali hiyo iweke kipumbele kwenye matibabu ya figo.

**HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA**

**TANGAZO KWA WADAIWA WA VIWANJA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia wananchi wote wanaodaiwa viwanja katika maeneo ya Mtumba, Michese, Nzuguni, Kitelela, Kikombo, Iyumbu, Nzuguni Bus Stand, Nala Industrial Area, Njedengwa Investment Area, Nala, Chahwa, Iyumbu New Town Centre, Mahomanyika, Vikonje, Nala Chigongwe, Ihumwa, Mapinduzi, Medeli, Nala Iugala, Nala Segu kukamilisha malipo ya viwanja hivyo mapema.

Mwananchi au taasisi itakayoshindwa kulipia kiwanja hadi kufikia tarehe 25 Machi, 2023 atambue kuwa kiwanja hicho kitauzwa kwa mteja mwingine ili kuboresha huduma katika Halmashauri bila kutoa taarifa yeyote kwa mteja wa awali.

**Tangazo hili limetolewa na:**

Joseph C. Mafuru
**MKURUGENZI WA JIJI**
**DODOMA**

MKURUGENZI WA JIJI
HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA
S.L.P. 1249,
DODOMA

217303602

# Buriani Richard Makore tutakumbuka ucheshi wako

**Na Joseph Mwendapole**

USIKU wa Jumanne Machi 7, majira ya saa 3:45 utabaki kwenye kumbukumbu ya maisha yangu nilipopata simu ya ajali iliyosababisha kifo cha rafiki yangu wa karibu Richard Makore.

Ni majira hayo ya saa 21: 45 nilipopokea simu kutoka kwa rafiki yangu mmoja akinipa taarifa mbaya ya ajali ya basi la Sheratoni lililokuwa likitoka Mwanza kuelekea Geita.

Mtu huyo aliniuliza 'Mwendapole una habari rafiki yako Makore amepata ajali mbaya?' Nikamuuliza 'imetokea wapi na hali yake ikoje?' Akaniambia hafahamu lolote ila ameambiwa ajali ile ni mbaya sana na watu wameumia sana.

Mtu huyo aliniambia kwa kuwa ilikuwa usiku, angetafuta habari kukicha kwani watu wengi hawakufahamu alikokuwa Makore na hata simu yake ya mkononi ilikuwa ikipigwa inapokewa na mtu mwingine. Kumbe wakati tunazungumza yote hayo, Makore alishatangulia mbele za haki.

Nilimuuliza kwani 'huyo mtu aliyeshika simu ya Makore amejitambulisha kama nani na amesema lolote kuhusu aliko Makore?' Akajibu kwamba amejitambulisha kama mmoja wa majeruhi wa ajali hiyo na alikuwa wodini na hakujui alikokuwa mwenye simu hiyo.

Hali hiyo ilinishtua kidogo na kuanza kuona kwamba sasa lolote linaweza kuwa limetokea kwa ndugu yangu Makore, kwani kama angekuwa majeruhi tungeweza kuongea naye akiwa wodini au hata wenzake wangesema wako naye.

Ghafla nilipokea simu nyingine kutoka kwa Mary Geofrey, mwandishi wa Nipashe, naye likawa hilohilo, 'Mwenda una habari Makore amepata ajali huko Geita akitokea Mwanza?' Nilimwambia 'nimepata taarifa ila tusubiri taarifa rasmi mapema asubuhi'.

Kwa kweli nililala usingizi wa mang'amung'amu na ilipofika asubuhi sikutaka kuchungulia kwenye kundi letu sogozi (WhatsApp) kujua kinachoendelea maana taarifa nyingi zilikuwa zinatofautiana.

Kulipokucha nikamwambia mke wangu 'sitaki kuingia kwenye kundi letu sogozi muda huu, ngoja niende mazoezini', nitaangalia wakati ninaondoka majira ya saa nne asubuhi angalau kunaweza kuwa na taarifa rasmi ya aliko rafiki yangu Makore.



Baadhi ya maofisa wa polisi, waandishi wa habari na wananchi wa mtaa wa Lumala, Kata ya Pansians, wakishiriki kulibeba jeneza lenye mwili wa marehemu Richard Makore, kwa ajili ya kulipakia kwenye gari ili kusafirishwa kwenda nyumbani kwao, Kijiji cha Remng'orori wilayani Serengeti mkoani Mara kwa maziko, baada ya kuagwa jijini Mwanza jana. **PICHA: VITUS AUDAX**

Kweli, baada ya mazoezi nilijitayarisha na kuingia kwenye gari nikiwa bado sijaingia kwenye kundi letu sogozi, lakini wakati nakaribia kuwasha gari simu iliita na nilipoangalia alikuwa ni Mary.

Nilipata wasiwasi lakini nilijipa moyo na kuipokea na moja kwa moja bila hata salamu Mary aliniambia Mwenda umepata taarifa? imethibitishwa kwamba Rich ametutoka.

Nilishikwa na bumbuwazi na sikujua cha kufanya na nilikaa kwenye gari dakika 10 mpaka mke wangu alipokuja kuchungulia kwanini nimekaa muda mrefu bila kuondoka.

Nilimjibu neno moja tu, 'mke wangu tuishi kwa upendo, 'life is too shot', imethibitishwa kwamba Makore amefariki dunia.

Mke wangu alibubujikwa na machozi kwani ni mtu aliyemfahamu vyema Makore. Familia yangu na ya Makore tulikuwa karibu sana kwani kuna wakati wao walikuja kwetu wakati wa sikukuu na sisi tulikwenda kwake Goba sikukuu inayofuata kabla hayahamishiwa Mwanza kikazi miaka michache iliyopita.

Makore atakumbukwa kama mtu asiye na gubu na mtu na ambaye alikuwa mwepesi kwenye utani na ambaye unaweza kumtania utakavyo na yeye kuishia kucheka tu.

Mwezi Agosti mwaka jana, nikiwa kwenye shughuli zangu mkoani Mwanza, nilimtafuta na tukakaa kwenye moja ya hoteli jirani kabisa na Uwanja wa Furahisha, tulizungumza mambo mengi ya maendeleo na ya familia.

Moja ya mambo aliyoniambiwa ni kwamba hataraji kurudi tena kuishi Dar es Salaam kwani amepapenda Mwanza na atawekeza kwenye mkoa huo kwa maisha yake yote.

"Mimi kwetu ni hapo Serengeti ambapo ni saa chache tu kutoka hapa, hata nikifa watu hawatapata shida ya gharama za kunisafirisha. Nitakaa Mwanza, sitorudi tena kwenye foleni zenu Dar es Salaam," nukuu ya kauli yake ninayoikumbuka.

Kwa kuwa Makore ni mtu wa Mkoa wa Mara na mimi ni Mhangaza (watani), tunapokaa sehemu huwa utani unachukua sehemu kubwa ya mazungumzo yetu, hivyo baada ya kutoa kauli hiyo nilimwambia 'ukifa mke wako atakuwa halali yangu'.

Nilipomwambia hivyo, Makore alicheka sana na kwa kweli nilikuwa ninapenda mno aina yake ya kucheka, ndiyo sababu nilikuwa nikimtania mara nyingi hasa kuhusu mke wake ili nione kicheko chake.

Mmoja wa marafiki wa karibu wa Makore, Mashaka Mgeta, aliandika kwenye ukurasa wake wa Facebook 'Mdogo wangu **RICHARD MAKORE** ni vigumu kuamini kwamba umetangulia kwa kulala usingizi wa milele. Lakini uliniambia hivi karibuni kwamba unajenga nyumbani Serengeti ili hata umauti ukikukuta usiadhirike utakapokwenda kulazwa. Mwendo umeumaliza. Pumzika kwa amani rafiki yangu'.

Mwandishi wa ITV, Godfrey Monyo ni miongoni mwa watu wa karibu wa Makore ambaye walisoma darasa moja Chuo cha Uandishi wa Habari (TSJ) ambacho kwa sasa kinafahamika kama Shule Kuu ya Uandishi wa Habari ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (SJMC).

Monyo anamwelezea Makore kama mtu mwenye bidii darasani na kazini kwani ni mtu aliyependa kuona matokeo chanya kwa kila jambo analofanya na hakutaka kushindwa.

Anasema Makore akiwa darasani hakuwa mtu mwoga kuuliza maswali kwa walimu pale alipoona jambo hajalifahamu vyema na anakumbuka namna alivyokuwa akimhoji maswali mengi aliyekuwa mwalimu wao wa somo la uandishi wa habari, News Writing (Dk. Ayubu Rioba).

"Makore alikuwa anapenda sana kuhoji mpaka tukambatiza 'Bwana Maswali'. Mimi Makore, Vick Kimaro, Ikunda Erick ninakumbuka kwamba ni wanafunzi wa mwanzo kabisa kupata cheti cha IJMC baada ya kubadilika kutoka TSJ. Sisi tulianza kusoma TSJ lakini tukamaliza ikiwa IJMC," anasimulia.

Monyo anasema Makore ni mtu mwenye upendo wa kusaidia watu asiyependa kuona mtu anakwama kwa kitu ambacho yeye anaweza kumsaidia.

Anasema hata darasani kwao alikuwa msaada mkubwa kwa wanafunzi wenzake wakati wa mijadala ya wanafunzi kwani alikuwa mstari wa mbele kuelezea kile anachokifahamu ili kuwapa maarifa wenzake.

Monyo anasema walipomaliza IJMC, Makore alitangulia kufanya mafunzo ya vitendo Nipashe mwaka 2001 na yeye kuungana naye baada ya miezi mitatu kufanya mafunzo kwa vitendo.

"Nilimkuta Makore Nipashe akiwa ameshayazoea mazingira ya pale na nakumbuka hata habari yangu ya kwanza kabisa kutoka kwenye gazeti la Nipashe ilikuwa ya kipindupindu, nilipotoka jiji kurudi chumba cha habari alinipokea,

"Wakati huo hata kuchapa habari kwenye kompyuta sikuwa mahiri, yeye ndiye alinisaidia kuichapa na kurekebisha kasoro zilizokuwapo na siku iliyofuta nilipoiona kwenye gazeti nilifurahi sana na tangu wakati huo Makore na Ikunda wakawa wakufunzi wangu pale Nipashe.

Rafiki mwingine wa karibu, Hellen Mwango anasimulia namna Makore alivyotoa mchango mkubwa kumjenga kitaaluma kwa mawazo na kwa kuhariri habari zake.

Hellen anasema Julai 2004, akitokea Chuo cha Uandishi wa Habari (TIME), alikwenda Nipashe kufanya mazoezi ya vitendo ambapo siku yake ya kwanza alipangiwa kwenda kutafuta habari na Richard Makore.

"Mimi na Makore siyo watani lakini mtu aliyetufahamu angefikiri hawa ni watani maana tulikuwa muda mwingi tunataniana. Kuna wakati tulikwaruzana lakini haipiti siku utatukuta pamoja kwa sababu Makore hakuwa na kawaida ya kuweka sumu moyoni," anasimulia Hellen.

"Makore Februari 2022 ulinitumia Sh. 25,000 kwa sababu nilikuwa ninaugua nyumbani, ulinipangia kabisa ninunue mchele na sukari, umeniachia deni kubwa kwa mkeo Fransisca na watoto wako, tangulia Rich," alisema Hellen.

Sanula Athanas, Mhariri Msanifu wa Nipashe anasema atamkumbuka Makore kama mmoja kati ya waandishi mahiri wa habari za jinsia nchini.

"Hili linathibitishwa na ubora wa kazi zake kwenye eneo hili. Kwenye Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), kabla hatujampangia majukumu mengine mkoani Mwanza, Makore alishinda tuzo nyingi katika kipengele hiki (Habari za Jinsia).

"Ilifika kipindi Tuzo ya Habari za Jinsia upande wa magazeti ilionekana kama inaandaliwa kwa ajili yake. Alikuwa mwandishi mahiri kwenye eneo hili," anasema.

# Chongolo kuwaweka kitimoto mawaziri

**Na Augusta Njoji,** KITETO



KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo (pichani) amesema Jumatatu wiki ijayo ataanza kuwaweka 'kitimoto' baadhi ya mawaziri kutokana na kero alizozibaini katika ziara yake mikoa ya Singida na Manyara.

Kero hizo ni pamoja na mwingiliano wa wanyamapori kwenye makazi ya watu, matatizo ya maji, huduma za afya, ubovu wa barabara, ruzuku ya mbolea na uhitaji wa chakula cha bei nafuu.

Akiwa ameambatana na wajumbe wawili wa sekretarieti ya CCM; Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Sophia Mjema pamoja na Katibu wa NEC, Idara ya Oganizesheni, Issa Gavu, malalamiko mbalimbali yaliibuliwa na wananchi kwenye maeneo hayo.

Akizungumza jana Kijiji cha Ndaleta baada ya msafara wake kuzuiwa na wananchi eneo hilo akielekea Kiteto mkoani Manyara, Chongolo alisema amepokea kero za wananchi kwenye maeneo mbalimbali na kuanzia Jumatatu wiki ijayo, baada ya kuhitimisha ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2020 hadi 2025, ataanza kuwaita kuzungumza nao.

"Suala la tembo sio zuri, nisiseme maneno mengi hayatatui tatizo, ninarudi waliko mawaziri wa hizo wizara nitakwenda kuwaita kuanzia Jumatatu wiki ijayo wanieleze wanafanya nini.

"Kwanza hao wanaonufaika na tembo kwa upande wa hifadhi ndio wanaopaswa kuhangaika kuwadhibiti wasilete madhara na yanayopatikana yawe na fidia ya ukweli sio hadithi," alisema.

Chongolo alisema lazima uundwe mfuko wa fidia wa uharibifu wa wanyamapori na uhusishe maeneo ya hifadhi yanayozunguka vijiji husika na viwe kwenye kamati ya mfuko huo, ili mjadala wa fidia usiwe hadithi, bali utengenezewe utaratibu wa kuweka fedha asilimia fulani kulingana na mapato ya hifadhi.

Alisema kila eneo alilopita lenye wakulima wazuri wamelalamikia uharibifu unaofanywa na wanyamapori hususan tembo, hivyo ni wakati wa serikali kuchukua hatua ya kuwadhibiti na kutoa fidia stahiki kwa wakulima.

Kuhusu barabara, Chongolo alisema atateta na Rais Samia Suluhu Hassan kuhusu barabara ya Arusha-Kiteto hadi Kongwa, ili iingizwe kwenye kipaumbele na ijengwe kwa kiwango cha lami.

Kuhusu kero ya maji, alisema leo anatarajia kukutana na Waziri wa Maji, Jumaa Aweso wilayani Babati na atatoa majibu ya kero ya maji Manyara ikiwamo Kata ya Ndaleta.

Pia alielekeza kuwa ndani ya siku 14, Waziri au Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi wawe wamekwenda kutatua mgogoro unaowakabili wananchi wa eneo hilo na si kukaa ofisi.

Wakitoa kilio chao kwa Chongolo, baadhi ya wakazi wa Ndaleta akiwamo Athuman Ramadhani, walisema kata hiyo inakabiliwa na tatizo la maji na ubovu wa barabara unaosababisha wakati wa masika kuuza mazao kwa bei ya hasara.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Ndaleta, Juma Bakari alisema mwaka 2021 kijiji kilifanya tathmini ya kulipa fidia uharibifu uliofanywa na tembo ambapo majina yalikwenda, lakini mwaka 2022 yalirudi na kutakiwa namba za NIDA, ili fedha zitoke hadi sasa hakuna lililofanyika na tembo bado wanasumbua.

Abdallah Mfaume alisema kero kubwa ni Hifadhi ya Indema iliyo chini ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) wilayani Kiteto ambayo imewanyang'anya mashamba, kuwapiga na kupora mali zao licha ya viongozi wa mkoa kuwaruhusu kufanya shughuli za kilimo.

Alisema ni miaka tisa sasa hawafanyi shughuli za kilimo na kushindwa kusomesha watoto wao.

Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere alikiri kero hiyo ya tembo kusumbua eneo hilo na shule ya sekondari ambayo wanyama hao wanaingia hadi kwenye mabweni.

Alisema suala la fidia kutoka WMA limekuwa kero na upande wa hifadhi hawana utaratibu huo.

Kuhusu kuporwa mashamba na WMA, alisema walipanga kwenda na Naibu Waziri wa Ardhi na suala hilo linamuumiza kiasi cha kuona aibu kutokana na kuchukua muda mrefu pasi na kupatiwa ufumbuzi.

Awali Mbunge wa Simanjiro, Christopher Ole Sendeka, alisema wananchi waendelee kukiamini chama na kitashughulikia kero zao ipasavyo.

"Suala la tembo kuwa kero wanatoka Hifadhi ya Tarangire, Pori la Akiba la Mkungunero na hifadhi ya Indema-WMA iliyopo eneo la Makani, wanakuja kwenye maeneo haya, katika msimu kama huu tembo asilimia kubwa wameondoka kwenye hifadhi ya taifa wamekuja kwenye mapori ya Wilaya ya Simanjiro na Kiteto inahitajika kufanyika utafiti kuna majani hayapo hifadhini kwa sasa kama migunga," alisema.

Alisema suala hilo linahitaji maelekezo ya chama kwa serikali ili uharibifu unaotokea fidia itolewe kulingana na thamani ya mazao yaliyoharibiwa.


## NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **STICK UP AUCTION MART,J&J RECOVERIES,LIMITED,HOLLYNESS AND RESPISHERS CO.LTD, MUDU.CO.LTD and MASE INTERNATIONAL LIMITED** Kwa idhini tuliyopewa na **FINCA MICROFINANCE BANK LTD** tunatoa muda wa siku 14 kwa wadaiwa walioorodheshwa kwenye jedwali hapo chini wawe wamelipa madeni wanayodaiwa na FINCA MICROFINANCE BANK LTD. Kinyume na hapo tutalazimika kuuza kwa njia ya mnada wa hadhara mali walizoweka kama dhamana ya mkopo. Tarehe za kufanya minada zitatolewa kwa njia ya vipeperushi na magari ya matangazo kwenye sehemu dhamana zilipo.

| | NOTISI YA KULIPA DENI NA TANGAZO LA MNADA WA HADHARA | | |
|---|---|---|---|
| | STICK UP AUCTION MART | | |
| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA | MAHALI ILIPO DHAMANA |
| 1 | Tadei Kapinga Kapinga | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Pongwe- Tanga |
| 2 | Rukia Hamza Mafua | Nyumba yenye Hati miliki kiwanja no.144, kitalu | Michungwani-Tanga |
| 3 | Begge Hemedi Begge | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mwahako-Tanga |
| 4 | Shehe Mzee Mohamed | Nyumba yenye mkataba wa mauziano mali mdhamini Agness John Masanyika | Neema- Tanga |
| 5 | Mashaka I Panduka | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | mbasa- Ifakara |
| 6 | Naftari M Yusuph | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Kaporo- Ifakara |
| 7 | Samweli B Ubongo | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Katindiuka- Ifakara |
| 8 | Evod E Shio | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Ihomwe-Mikumi-Ifakara |
| 9 | Moses Maganga shija | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | katindiuka- Ifakara |
| 10 | Lonard Rock Michael | Nyumba yenye hati miliki no.51, kitalu k | Matonga-Ifakara |
| 11 | Godfrey Matei Mwacha | Nyumba yenye mkataba wa mauzizno | Kihonjo- Ifakara |
| 12 | Juma R Sanze | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Mang'ula- Mwaya-Ifakara |
| 13 | Tatu K Tungupup | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Mahautanga-Ifakara |
| 14 | Egidi Egidi Ngasoma | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Kiningi'na-Ifakara |
| 15 | Mohmemed Michael Kutunguku | Nyumba yenye leseni ya makazi no.94, kitalu M | kibaoni- Ifakara |
| | J & J RECOVERIES | | |
| 16 | RAMADHANI JUMA KILAZA | Nyumba yenye Hati miliki kiwanja no.50, kitalu L na kiwanja chenyehati miliki no.166, kitalu A | Kiwanja cha ndege and Mkundi-Morogoro |
| 17 | LAZARO ANDREW MAGOSHO | Nyumba yenye Mkataba wa mauziano- Mali ya James George Mtundu | Lukobe- Morogoro |
| 18 | HUSSEIN KHALIFA ISSA | Nyumba yenye Mkataba wa mauziano | Mafisa- Tungi-Morogoro |
| 19 | SHAKILLY GAUDENSI ROCKY | Nyumba yenye Mkataba wa mauziano | Dakawa-Morogoro |
| 20 | ALEX MTESIGWA BULENGA | Nyumba yenye Mkataba wa mauziano | Kihonda -Magorofani-Morogoro |
| | HOLLYNESS AND RESPISHERS CO.LTD | | |
| 21 | Daudi Mwaibofu | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Itiji- Mbeya |
| 22 | Ainaswe Mallya | Nyumba Yenye mkataba wa mauziano | Tunduma- Mbeya |
| 23 | Hemed Sain | Nyumba yenye Mkataba wa mauziano | Tunduma- Mbeya |
| 24 | Witu Mwandunga | Pagale lenye mkataba wa mauziano | Uyole-Mbeya |
| 25 | Efraim Yuda Govela | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Itende- mbeya |
| 26 | Ambele A Mwangopola | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Iyela-Mbeya |
| 27 | Fidea A Mbogela | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Uyole-Mbeya |
| 28 | Neema H Ambonisye | kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Mbalizi- mbeya |
| | MUDU CO .LTD | | |
| 29 | Abubakari Zuberi Karata | Gari aina ya Nissan X - Trail yenye namba za usajili no. T 964 DDZ | Tegeta- Dar es salaam |
| 30 | Chapewa Patrick Mwisua | Pagale lenye mkataba wa mauziano | Isakalilo- Iringa |
| | MASE INTERNATIONAL LIMITED | | |
| 31 | Winifrida Baritazari Swedeka | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Nyansaka-Mwanza |
| 32 | Antony M Gereshon | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | kanyama- Mwanza |
| 33 | Mwita E Bange | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Nyahingi- mwanza |
| 34 | Selema A Selema | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Mahina- mwananchi-Mwanza |
| 35 | Ndera Abnel Mwita | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Lumala- Mwanza |
| 36 | Charles M Boniphace | Kiwanja chenye hati miliki no.225, kitaluA | kitundu-Geita |
| 37 | Theopister Simeo Kiberinde | Kiwanja chenye mkataba wa mauziano | Butego-Lumasa- katoro |
| 38 | Jenifer Erasto Mlimba | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Mawani- Katoro |
| 39 | Ladslaus kasana | Nyumba yenye hati miliki kiwanja no.36, kitalu J na kiwanja chenyehati miliki no.166, kitalu A | Msalala-Geita |
| 40 | Enos Jonas Damas | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Nyantorontoro- Katoro |
| 41 | Zuhura Hassan Mwishehe | Nyumba yenye mkataba wa mauziano | Msalala-Geita |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Ukaguzi unaruhusiwa kuanzia tarehe ya tangazo hili.
2. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
3. Mnunuzi atayeshinda anapaswa kulipa 25% ya bei aliyofikiwa siku ya mnada, na 75% iliyosalia atalipwa kulingana na makubaliano ya benki na mnunuzi.
4. Gharama zozote ikiwemo kubadilisha Hati miliki (transfer of ownership), na kumtoa mtu kwenye nyumba/eneo lililouzwa ni la mnunuzi.
5. Mnada utafanyika mahali ambapo dhamana zilipo na si vinginevyo.

217315702

KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NAMBA

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Stick Up Mart**
**S.L.P Arusha**
**Namba za simu: 0786559593**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**J&J Recoveries**
**S.L.P Dar es Salaam**
**Namba za simu: 0714292260**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Jada Investment Limited**
**S.L.P Dar es Salaam**
**Namba za simu; 0788493699**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Hollynes and Respishers Co.Ltd**
**S.L.P Mbeya**
**Namba za simu: 0762058614**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MUDU ,CO.LTD**
**S.L.P Dar es salaam**
**Namba za simu: 0768672367**

**NA**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**MASE INTERNATIONAL LIMITED**
**S.L.P MWANZA**
**Namba za simu: 0710885084**

**Finca Microfinance Bank Ltd**
**P.O. Box 78783**
**Namba za simu: 0768790399, 0754774949**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ushauri wa Rais Samia kwa wanawake uzingatiwe

**JUZI** wakati Rais Samia Suluhu Hassan, akihutubia kongomano la Baraza la Wanawake wa Chadema (BAWACHA), aliwataka kutumia nguvu ya chama chao kuungana na kila chama cha siasa kumkomboa mwanamke wa Tanzania.

Wito huo wa rais unaonesha alivyo na nia ya kuwaunganisha wanawake bila kujali itikadi zao za kichama ili kumkomboa mwanamke na madhila ya ukandamizaji, unyanyasaji na udhalilishaji.

Lengo la rais ni kuona mwanamke wa kitanzania anathaminiwa na kupewa haki kama mwingine yeyote duniani, kama alivyosema changamoto hazichagui dini, kabila wala itikadi ya kisiasa.

Kupitia kongomano hilo Rais Samia alikuwa anatoa ujumbe kwa wanawake wote kutumia Siku ya Wanawake Duniani kutathmini maendeleo yao na changamoto wanazokabiliana nazo kisiasa, kiuchumi na kijamii ili kupata maridhiano ya haki zao katika usawa wa kijinsia.

Kwa kuonesha kuwa yeye ni rais wa Watanzania wote bila kujali itikadi zao kisiasa, dini au kabila, aliwataka kufanya kazi kwa pamoja na kushikamana ili kukuza siasa za kistaarabu na za kusikilizana kuleta heshima kwa taifa na kustawisha uchumi.

Juhudi zake za kuhakikisha maridhiano kisiasa na kuunganisha taifa zimeleta matumaini makubwa ya mageuzi ambayo yameweka msingi mzuri katika mustakbali wa demokrasia na maendeleo ya taifa.

Rais Samia ameweka alama kubwa nchini kwa kuwa kiongozi wa kwanza kutoka chama tawala kukubali kuwa mgeni rasmi katika kongamano lililoandaliwa na wanawake kutoka chama cha upinzani.

Kukubali kwake ni kuonesha kuwa upinzani sio uadui bali ni sehemu ya kupeana mawazo, ubunifu yatakayosaidia kuipeleka mbele nchi kimaendeleo.

Malumbano hata siku moja hayawezi kuleta maendeleo kazi yake ni kuyadidimiza, badala ya watu kufikiria njia za kuleta mafanikio watakuwa wanawaza malumbano na mfarakano utakaosababisha nchi kurudi nyuma kiuchumi.

Wanawake ni taifa kubwa ndio maana Rais Samia amezungumza hayo katika kongomano hilo ili waweze kupata ujumbe na kubadilika.

Kuwa kwenye vyama tofauti vya siasa hakumaanishi kuwa ni uadui, kinachoshindaniwa hapo ni sera nzuri za chama zitakazoleta mabadiliko ambayo wananchi watanufaika nayo kwa maendeleo yao.

Katika mkutano huo wa BAWACHA, Rais Samia alisema wazi kuwa ulikuwa na sura ya kisiasa zaidi na anaamini kuwa atapata jukwaa lingine aseme yake yote ambayo serikali yake imeyafanya ndani ya kipindi cha miaka miwili ambacho amekuwa kiongozi wa nchi.

Alipoingia madarakani Rais Samia, alitaka yale yote ya maendeleo yaliyoanzwa na mtangulizi wake na ambayo bado hayajakamilika, yaendelee bila kusimama ndio maana aliingia na kaulimbiu ya 'Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kazi iendelee'.


Kujiamini kwake na uhusiano wake mzuri na mataifa ya nje kumemwezesha kukubalika na kupata fursa nyingi za kuendeleza miradi ya kimkakati.

Ushirikiano wake na mataifa mengine, umeitambulisha Tanzania na kuifanya itembelewe na wageni wengi na wawekezaji wanaotaka kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya kimaendeleo.

Rais Samia peke yake hawezi kutimiza yote anayokusudia kuyatekeleza kama hatapata ushirikiano mzuri kutoka kwa wanawake wenzake na Watanzania wote kwa ujumla.

Umuhimu wa wanawake kushikamana na kuwa na umoja ni jambo la msingi kwa maendeleo ya nchi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com





## Muungwana Lazima Nilonge

# Tufahamu uchakachuaji huu wa mbolea, unageuka mzigo serikalini, kwa mkulima

Na Sabato Kasika

**KILIMO** ndio uti wa mgongo wa taifa! hilo halina ubishi, ingawa kuna ukweli kutumia jembe nako ni mtihani. Inaelezwa kuwa Watanzania zaidi ya asilimia 80, wanajishughulisha nacho.

Wakati kilimo chenyewe kikiwa bado ni cha kusuasua, sasa kimeingiwa na hujuma ambazo kama hazitadhibitiwa haraka, wakulima wataendelea kuumia, wakitumia nguvu hata wasipate mazao ya kutosha.

Serikali imejitahidi kuwasaidia wakulima kuzalisha kwa ufanisi, huku bei ya mbolea za kupandia zikipatiwa unafuu lakini baadhi ya waliopewa jukumu la kusambaza mbolea wanahujumu.

Kwa mfano, serikali imeshusha bei ya mbolea ya kupandia aina DAP kutoka shilingi 140,000 za awali hadi kufikia shilingi 70,000, mbolea ya kukuzia aina ya UREA kutoka shilingi 150,000 ya awali hadi shilingi 70,000. Kwa sasa wameibuka baadhi ya watu wanaouzia wakulima mbolea feki, huku wengine wakiweka mchanga katika mifuko ya mbolea, kitendo kinachoweza kuwafanya wakulima waamini kuwa ni mbolea na kumbe sivyo.

Wakala na wafanyabiashara wanaofanya hujuma hizo, wameshakamatwa, hivyo kukamatwa kwao, kungetosha kuwaonyesha kuwa serikali inafuatilia kwa karibu suala la kilimo, kwani kimsingi ndio uti wa mgongo wa taifa.

Fikiria serikali imepunguza gharama ya mbolea ili kusaidia wakulima kupata mavuno mengi, halafu wanajitokeza baadhi ya watu wanafanya hujuma, ninadhani watu wa aina hiyo waendelee kubanwa zaidi.

Serikali imetoa fedha nyingi kwa ajili ya kubeba dhamana ya ruzuku ya mbolea ya wakulima. Halafu wanajitokeza baadhi ya wakala na wafanyabiashara wanahujumu jitihada hizo.

Hujuma hizo zinakwamisha juhudi za serikali, wakulima na hata maendeleo ya taifa kwa ujumla, kwani uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara unaweza kuwa duni kutokana na kukosa mbolea inayotakiwa.

Kukutwa mifuko 776 yenye mchanga katika ghala la kuhifadhia mbolea ya ruzuku mkoani Njombe, inayodhaniwa huenda inatumika katika kuchakachua mbolea na kuuzwa kwa wakulima, inaweza kuwa ni hujuma.

Katika mazingira hayo, haijulikani ni wakulima wangapi wameuziwa mifuko ya michanga wakiamini ni mbolea. Hapa inaonyesha wahusika watakuwa wamejinufaisha kwa jasho la wakulima.

Serikali ilianzisha mkakati wa ugawaji ruzuku ya mbolea, kwa lengo la kuwakwamua wakulima na kuongeza kasi uzalishaji katika sekta hiyo inayotegemewa na wananchi wengi.

Rais Samia alishawahi kubainisha hayo, alipohudhuria mkutano wa jukwaa la uchumi duniani uliofanyika nchini Uswisi na kuelezea jinsia ambavyo sekta ya kilimo kwa Tanzania inavyotarajia kukua.

Hatua hiyo inachagizwa na kile alichosema mipango mikakati inayotekelezwa na serikali, na kwamba ifikapo mwaka 2030, sekta ya kilimo itasonga mbele kwa asilimia 30, ikilinganishwa na ya sasa ambayo ni asilimia 3.6.

Baadhi ya mambo ambayo Rais aliyaainisha na yanayotazamwa kama nguzo, katika kuchochea ukuaji huo, ni pamoja na mageuzi yanayoendelea kufanywa ndani ya sekta ya kilimo kama vile uanzishwaji mpango wa vijana kujikita kwenye kilimo na ongezeko la kiwango cha bajeti katika sekta hiyo.

Kwa mujibu wa Rais, bajeti hiyo ya kilimo kwa mwaka wa fedha 2022- 2023 imeongezeka mara nne ikilinganishwa na ile iliyopita. Ongezeko hilo limeifanya serikali kuwa na uwanja wa kuanza kutoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima.

Wakati serikali ikitoa ruzuku ya mbolea kwa wakulima, wanaibuka wajanja wachache ambao wanaamua kuwauzia mbolea feki kitendo ambacho ni wazi kinakwamisha juhudi za serikali na za wakulima wenyewe.

Hujuma nyingine zinazodaiwa kufanywa na baadhi ya watu hao, ni utoroshaji wa kimagendo wa mbolea kwenda kuuzwa katika mataifa ya jirani huku wakulima wa ndani wakiuziwa mchanga.

Ni kweli kwa miaka mingi sekta ya kilimo imekuwa ikijikongoja, kutokana uwekezaji mdogo wa muda mrefu, lakini safari hii wakulima walikuwa wameshapata matumaini mapya, kwa jitihada zilizochukuliwa na serikali.

Lakini inasikitisha kuona baadhi ya watu wakihujumu jitihada hizo, kwani bila kuchukuliwa hatua za kisheria, wanaweza kusababisha lengo la serikali la kutaka kuinua sekta ya kilimo kukwama.

# Bayport yasaidia matibabu ya watoto 300 Muhimbili

**Na Maulid Mmbaga**

TAASISI ya Kifedha ya Bayport Financial Services imetoa Sh. milioni 15 kusaidia gharama za matibabu kwa watoto 300 wanaotibiwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Taasisi hiyo ilitoa msaada huo juzi mkoani Dar es Salaam wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Akizungumza katika makabidhiano ya hundi ya fedha hizo, Mkuu wa Kitengo cha Utawala wa Bayport Financial Services, Suzan Kolimba, alisema taasisi yao iliguswa na changamoto wanazopitia watoto, hali iliyowasukuma kutoa msaada huo.

Alisema kuwa tangu mwaka 2006 walipoingia kwenye sekta ya mikopo ya fedha kwa watumishi wa umma, wamekuwa wakitoa misaada mbalimbali kama sehemu ya kurudisha kwa Watanzania waliochagua kuhudumiwa na taasisi hiyo.

"Hali hii inatufanya tuone thamani ya Watanzania wanaoendelea kuichagua Bayport kupata huduma za mikopo ya fedha, ndio maana tunaona haja ya kujitolea msaada wa matibabu kwa watoto hawa 300 hapa Muhimbili," alisema Suzan.

Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Prof. Mohamed Janabi, aliwashukuru Bayport kwa kusaidia gharama za matibabu kwa watoto hao na kuwataka waendelee kujitolea kwa jamii kwa manufaa ya taifa.

"Huu ni msaada mkubwa kwa watoto hawa, hivyo Bayport mwendelee kujitolea kwenye jamii yetu kwa sababu ni jambo zuri mno mmefanya.

"Sasa wazazi na walezi wa watoto hawa angalau watakuwa wamepungukiwa na gharama za matibabu kwa sababu nyie mmejitokeza kuwasaidia," alisema Prof. Janabi.




Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Prof. Mohamed Janabi (katikati), akiwa na baadhi ya watumishi wa hospitali hiyo, baada ya kupokea mfano wa hundi ya Sh. milioni 15 kutoka kwa wafanyakazi wa Taasisi ya Bayport Financial Services, kwa ajili ya kusaidia matibabu kwa watoto wenye changamoto ya gharama za matibabu hospitalini hapo, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tanzania yafungua milango uwekezaji mabadiliko tabianchi

**Na Jenifer Gilla,** DOHA

MAKAMU wa Rais, Dk. Phillip Mpango, amesema Tanzania imeweka kipaumbele uwekezaji katika maeneo muhimu ya kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, ikiwamo nishati ya jua na upepo, usimamizi bora wa taka pamoja na teknolojia rafiki kwa mazingira.

Mpango aliyasema hayo jana aliposhiriki majadiliano ya viongozi wa juu wa mataifa mbalimbali katika ajenda ya mabadiliko ya tabianchi katika Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDCs) unaofanyika Doha, nchini Qatar.

Aidha, Mpango alisema Tanzania inashuhudia athari zitokanazo na mabadiliko ya tabianchi ikiwamo matukio makubwa ya ukame na mafuriko, hali ya mvua isiyotabirika, kupanda kwa kina cha bahari na baadhi ya visiwa kuzama na kusababisha uhaba wa chakula, migogoro ya kijamii pamoja na kupanda kwa gharama za maisha. Pia Tanzania inakadiriwa kuwa na hasara ya kiuchumi hadi kufikia Dola milioni 33.7 katika kipindi cha miaka kumi iliyopita kutokana na mafuriko.


Dk. Mpango alisema katika kukabiliana na hali hiyo serikali inachukua hatua mbalimbali, ikiwamo uchimbaji wa mabwawa kuhifadhi maji, kuhamasisha nishati safi ya kupikia, upandaji miti kila mkoa, kujenga kingo kando ya bahari kudhibiti mmomonyoko wa udongo, kuandaa mkakati wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi pamoja na mpango kabambe wa mazingira wa mwaka 2022-2032.

Katika hatua nyingine pia amekutana na kufanya mazungumzo na Rais wa Slovenia, Natasa Pirc Musar, yaliofanyika katika mji wa Doha nchini Qatar kando ya Mkutano wa Tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDCs).

Viongozi hao wamejadiliana masuala mbalimbali ya ushirikiano katika sekta za kimaendeleo pamoja na uhifadhi wa mazingira. Rais wa Slovenia aliikaribisha Tanzania kushirikiana kupata teknolojia rafiki kwa mazingira ambayo nchi hiyo imewekeza zaidi.

Mazungumzo hayo yamehudhuriwa na Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Saada Mkuya, Naibu Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki Balozi Mbarouk Mbarouk pamoja na Naibu Mwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Umoja wa Mataifa (New York), Balozi Dk. Suleiman Haji Suleiman. Makamu wa Rais yupo nchini Qatar kwa siku sita akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan, kwenye Mkutano wa tano wa Umoja wa Mataifa wa Nchi Zinazoendelea (LDC5).

**KABWELA** — **Na Fadhili Mohammed**



MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# TAARIFA KWA UMMA

## KUHUISHA TAARIFA ZA NAMBA YA UTAMBULISHO WA MLIPAKODI (TIN) NA NAMBA YA UTAMBULISHO WA TAIFA (NIN)

***Dar es salaam, 10 Machi, 2023***

Kwa mujibu wa mabadiliko ya Sheria ya Fedha ya mwaka 2022, Kifungu cha 22 cha Sheria ya Usimamizi wa Kodi (Sura 438) kinampa mamlaka Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kumsajili na kumpa Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN) kila Mtanzania mwenye umri wa miaka kumi na nane (18) na kuendelea ambaye amesajiliwa na kuwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) inayotolewa na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Sambamba na hilo, mabadiliko hayo ya Sheria yanamtaka kila mwenye TIN kuhuisha taarifa zake ili ziwiane na taarifa za NIN. Utekelezaji wa Sheria hii ulianza rasmi tarehe mosi Januari 2023.

Katika utekelezaji wa Sheria hiyo, TRA inapenda kuumbusha Umma kwamba, usajili wa TIN unafanyika kwa kutumia taarifa za NIN. Aidha, kila mwenye TIN ambaye alisajiliwa awali kwa kutumia vitambulisho tofauti na kitambulisho cha NIDA, anatakiwa kuhuisha taarifa zake za TIN ziendane na taarifa zilizopo kwenye NIN.

Ili zoezi la uhuishwaji wa taarifa hizi lifanyike kwa urahisi na wepesi, inashauriwa kwamba kila mwenye TIN ambayo bado haijahuishwa, kufika katika ofisi za TRA zilizo karibu naye akiwa na Namba ya Utambulisho wa Taifa (NIN) ili taarifa zake ziweze kuhakikiwa na kuhuishwa. Kwa wale wenye NIN lakini hawana TIN, wanaweza kufanya usajili wa TIN kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Mamlaka ya Mapato Tanzania.

Ikumbukwe kwamba huduma zote za utoaji wa TIN ni bure na rahisi. Kwa taarifa zaidi, tembelea Ofisi za TRA zilizo Karibu nawe au tumia mawasiliano yafuatayo:

**Tovuti** : **www.tra.go.tz**
**Namba za Simu bila malipo** : **0800 750 075 au 0800 780 078 au 0800 110016**
**WhatsApp** : **0744 23 33 33**
**Barua pepe** : **huduma@tra.go.tz au services@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

**Imetolewa na:**

**IDARA YA HUDUMA NA ELIMU KWA MLIPAKODI**
**TRA MAKAO MAKUU**

217316402



# DC awatangazia kiama wanaotekeleza vitendo vya ukatili

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Longido, Marco Ng'umbi, ametoa onyo kwa watu wanaojihusisha na vitendo vya ukatili wa kijinsia, akisema hatakuwa na huruma nao kwa sababu wanasababisha maumivu kwa jamii.

Aliyasema hayo jana katika eneo la Namanga wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, yalioandaliwa kwa ushirikiano wa Mtandao wa Polisi Wanawake (TFNET) na Shirika la Pingo's Forum.

"Sitacheka na watuhumiwa wa matukio yote ya ukatili na nawaonya bora waache mara moja maana hawatakuwa salama, nitawakamata tu popote watakapojificha," alisema.

Alisema wapo baadhi watu wanaendeleza vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia kwa kuwapiga picha za utupu wenza wao na kuzisambaza kwenye mitandao ya kijamii. Alisema wengine wakiingia katika mfarakano wanaanza kuchafuana katika mitandao kwa kutuma picha za utupu za mwenzake pamoja na maneno ya kashfa na kusababisha mhusika kujiua.

Alisema huo ni aina ya ukatili kama ulivyo mwingine, hivyo bora jamii ikabadilika na kuachana na tabia hiyo, kwani nao hawatabaki salama. "Wapo watu kazi yao ni kuchafua wengine, hili linasababisha mifarakano katika familia au vifo, ni jambo baya, nashauri watu watumie mitandao vizuri na siyo kuumiza wengine," alisema.

Alisema serikali itaendelea kutengeneza mazingira rafiki kwa wanawake ya kufanya biashara ili wapate fursa ya kujikwamua kiuchumi. Mkuu wa Kituo cha Polisi Namanga, SP. Erenesta Mwambinga, alisema kupitia kitengo cha dawati la jinsia wamekua wakitoa elimu kwa jamii ili kukomesha vitendo vya ukatili.

Alisema Wilaya ya Longido katika kipindi cha Januari hadi Desemba mwaka 2021 matukio ya ukatili 244 yaliripotiwa, huku mwaka 2022 yalikua 285, ikiwa ni ongezeko la matukio 41 sawa na asilimia 17.

Mkuu wa Kitengo cha Jinsia Pingo's Forum, Nailejileji Tipapu alisema kwa kushirikiana na wadau, wanaendelea kuelemisha wananchi wa pembezoni ili wanapokumbana na matukio ya ukatili waweze kutoa taarifa kwenye vyombo vya dola.




Meneja wa Barrick Tanzania, Dk. Melkiory Ngido (kulia) na Meneja Mkuu wa Mgodi wa Barrick North Mara, Apolinary Lyambiko (kushoto), wakiwalisha keki viongozi wa wanawake katika mgodi huo, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, mgodini hapo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TASAF yamwagiwa sifa utekelezaji wa miradi

**Na Allan Isack,**
ARUMERU

WAJUMBE wa kamati ya kusimamia ofisi ya viongozi wakuu kitaifa wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar, wameridhishwa na utekelezaji wa miradi ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), katika Halmashauri ya Meru mkoani Arusha.

Wajumbe hao wameridhishwa na ujenzi wa miradi ya TASAF waliyotekeleza kwa ufadhili wa umoja wa nchi zinazozalisha mafuta duniani (OPEC).

Akizungumza jana katika mkutano wa hadhara na wananchi wa Kandashe na wanufaika wa mradi huo,

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Machano Othman Said, alisema wajumbe wa kamati wamekwenda kuangalia miradi ya afya na elimu ili kujifunza namna ujenzi ulivyofanyika.

Kadhalika alisema Zanzibar miradi ya TASAF hasa ya ujenzi wa miundombinu imefanya vizuri, hivyo kwa kuwa serikali zimefanya vizuri wananchi wanapaswa kuzipongeza na kuziunga mkono.

"Ndugu wananchi ninawaomba tuhakikishe tunalinda miradi hii na inapotokea kasoro ndogo mfanyie ukarabati ili idumu kwa muda mrefu kwa maslai ya kizazi cha sasa na cha baadaye, alisema.

Makamu Mwenyekiti wa kamati hiyo, ambaye ni Mwakilishi wa Bumbwini, Mtumwa Pea Yusuph, alisema amefarijika kuona namna miradi hiyo ilivyotekelezwa kwa viwango na usimamizi bora na makini.

Mkuu wa Wilaya ya Arumeru, Emmanuela Kaganda, alisema serikali kupitia TASAF imetoa fedha za ujenzi wa miradi ili kuhakikisha wanaimarisha maisha ya wananchi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kandashe, Arodi Mafie, alisema awali wananchi walikuwa wakiteseka kupata huduma za afya kwa kuwa walitembea umbali mrefu hadi Wilaya ya Siha mkoani Kilimanjaro kufuata matibabu.

# DC aagiza wanaume washirikishwe mikopo ya asilimia 10

**Na Tumaini Mafie,**
ARUSHA

MKUU wa Wilaya ya Arumeru, Emanuela Kaganda, amezitaka taasisi na mashirika ya umma kuwashirikisha wanaume katika mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri zao ili nao wapate fursa ya kupata mikopo.

Aliyasema hayo jana jijini Arusha wakati wa ufunguzi wa kongamano la wanawake akimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Arusha, John Mongela.

Kaganda alisema wanaume wengi hawana fursa za mikopo ya vikundi kama ilivyo kwa wanawake na watoto wa kike.

"Nimeona zaidi wanawake na watoto wa kike wakiwa wanajumuishwa kwenye vikundi vya mikopo, lakini tunawasahau hawa watoto wa kiume, watakuja kukosa ujasiri wa kuwachumbia hawa watoto wetu wakike," alisema Kaganda.

Alisema kati ya vikundi vingi vinavyowezeshana, kinamama ndiyo wengi, hivyo wanaume wanakosa ujasiri wa kushindana na wanawake, hata katika mambo ya ujasiriamali hali ambayo siyo nzuri kwa mustakabali wa siku za baadaye.

"Katika wilaya yangu juzi nilienda kutoa mikopo kwa vikundi 37, lakini kati ya vikundi vyote hivyo ni vikundi viwili tu vilijitokeza vyenye wanaume, jambo ambalo kwa sasa nalipiga vita angalau kuwe na usawa wa kijinsia," alisema.


Akizungumzia kongamano hilo alisema hakuna nchi duniani, inayoweza kuendelea bila ushirikishwaji sahihi wa wanawake na wanaume, hivyo suala la ushirikishwaji ni muhimu.

Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Patrick Golwike, alisema taasisi zinazotoa mafunzo ya maendeleo ya jamii na jinsia zinapaswa kutazamwa kwa jicho la tatu kwa kuwa zinafanya kazi nzito.

"Ukitaka kuitengeneza Tanzania isiyo na ukatili, mwongozo unatokana na taasisi zinazotoa mafunzo ya maendeleo ya jamii na jinsia, hivyo ni za kuangalia kwa jicho la tatu, "alisema.

Kaimu Mkuu wa Chuo cha Maendeleo ya Jamii Tengeru, Dk. George Kinyashi, alisema kongamano hilo, limewaleta pamoja wanawake watatifi, kutoka Kituo cha Utafiti Taifa, kinachokuza ubunifu na kuratibu masuala mbalimbali ya utafiti za teknolojia, zinazowalenga wanawake kwa fursa za biashara.

Kongamano hilo liliandaliwa na Taasisi ya Maendeleo ya Jamii Tengeru, yenye kauli mbiu "Ubunifu na mabadiliko ya teknolojia ni chachu ya kuleta usawa wa kijinsia".





# Wafanyakazi wanawake GGML watoa vifaa tiba Halmashauri ya Geita

**Na Mwandishi Wetu, GEITA**

KIKUNDI cha wafanyakazi wa kike wanaofanya kazi katika Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML ladies) mjini Geita, wametoa msaada wa vifaa tiba ili kuwasaidia wajawazito na wazazi wanaojifungua kwenye Hospitali ya Nzela na Kituo cha Afya Kasota zilizopo Halmashauri ya Wilaya Geita.

Akizungumzia msaada huo uliotolewa juzi mjini Geita, Makamu Mwenyekiti wa kikundi hicho, Lina Sitta alisema wanawake wanaofanya kazi GGML wameguswa na changamoto za uhaba wa vifaa tiba kwenye vituo vya afya vilivyoko kwenye vijiji vinavyowazunguka.

"Tumeona kwa sasa tuanze na vijiji vya Kasota na Nzela ambavyo vipo karibu zaidi na mgodi wa GGML na tumekuwa tukiona changamoto ya kinamama kukosa sabuni, taulo za mama waliojifungua na nepi za watoto. Msaada huu tumeutoa maalum kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani," alisema.

Mganga Msaidizi wa Kituo cha Afya Kasota, Stanley Victor, aliwashukuru GGML Ladies kwa kutoa msaada huo, pia GGML kusaidia ujenzi wa maabara, nyumba ya mtumishi na jengo la mama na mtoto kituoni hapo.

"Mmeitendea haki Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu. Wagonjwa wengi walipo hapa wamefarijika sana kutokana na msaada huu," alisema.

Kaulimbiu ya Siku ya Wanawake Duniani mwaka huu ni 'Ubunifu na Mabadiliko ya Teknolojia: Chachu katika Kuleta Usawa wa Kijinsia'.



Mmoja wa wafanyakazi wanawake wa GGML kutoka Idara ya Uchakataji Dhahabu, Rehema Lusendamila (kushoto), akimjulia hali mgonjwa aliyelazwa kwenye Kituo cha Afya Kasota. Katikati ni Lina Sitta, Makamu Mwenyekiti wa Kikundi cha Wafanyakazi wa Kike wanaofanya kazi GGML. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Muleba yapokea bil. 60/- miaka miwili ya Rais Samia

**Na Titus Mwombeki,** MULEBA

KATIKA kipindi cha miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, Wilaya ya Muleba mkoani Kagera imepokea zaidi ya Sh. bilioni 60 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwenye elimu, afya, kilimo na uvuvi.

Katibu Tawala wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Greyson Mwengu, alibainisha hayo jana wakati wa maadhimisho ya siku 730 tangu Rais Samia alipoingia madarakani.

Maadhimisho hayo yaliambatana na maonyesho ya makala maalumu iliyoonyesha mafanikio yaliyotekelezwa na serikali katika kipindi cha siku hizo wilayani humo.

Alisema kuna baadhi ya miradi haikutekelezwa, mingine inaendelea hivyo itatekelezwa katika bajeti ijayo kwani wameshapeleka mapendekezo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Elias Kayandabila, alisema fedha hizo zimeelekezwa katika taasisi za serikali, ujenzi wa Hospitali ya Wilaya na ujenzi wa madarasa 457.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Muleba, Justus Magongo, alisema kuna baadhi ya miradi ambayo haijakamilika kwa wakati, huku akisema kuwa katika bajeti ijayo wamepeleka mapendekezo ili kuhakikisha miradi hiyo inatekelezwa kwa wakati.

Alisema Halmashauri ya Wilaya ya Muleba imeendelea kusimamia mikopo ya asilimia 10 kutoka mapato ya ndani ambayo imelegwa kwa kinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

# DC aagiza vikundi ujasiriamali vilivyokopeshwa kufuatiliwa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAKURUGENZI wa halmashauri mkoani Shinyanga, wameagizwa kuvifuatilia vikundi vya wajasiriamali ambavyo vimepewa mikopo ya halmashauri, ili kuona matumizi sahihi ya fedha hizo.

Mkuu wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, alibainisha hayo juzi wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Dunia. Mkude alimwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Christina Mndeme.

Alisema vikundi ambavyo vimekuwa vikinufaika na fedha za mikopo ya halmashauri ni vyema vikawa vinafuatiliwa ili kuona maendeleo yao kuliko kuachawa, mwisho wa siku vinakufa na fedha ya serikali zinapotea.

"Nawapongeza wakurugenzi kwa kuendelea kutoa fedha za mikopo ya asilimia 10 kwa vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu, ila naagiza vikundi ambavyo vinapewa fedha hizi za mikopo vifuatiliwe ili vifikie malengo yaliyokusudiwa ya kujikwamua kichumi," alisema Mkude.

Mkude aliwataka wanawake kupinga masuala ya mila na desturi zenye madhara, ambazo zimekuwa zikiwakandamiza na kusababisha kukosa fursa mbalimbali ikiwamo kugombea nafasi za uongozi. Pia alisisitiza wananchi wa mkoa huo kuendelea kuchukua tahadhari dhidi ya kujikinga na maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU), ugongwa wa corona ikiwamo kupata chanjo.

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake mkoani Shinyanga, Dk. Regina Malima, alitaja vikwazo ambavyo vinawakabili wanawake kushindwa kuinuka kiuchumi kwamba ni ukosefu wa rasilimali fedha, uelewa mdogo masuala ya ujasiriamali na wengine kushindwa kutumia fursa za mikopo.

Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Shinyanga, Tedson Ngwale, alisema katika uwezeshaji wanawake kiuchumi kipitia fedha za mikopo kimeshatolewa Sh. bilioni 2.5 kuanzia mwaka 2022 hadi Machi mwaka huu.




Ukurasa 12

KINAMAMA WANAPOJIVUNIA WIKI YAO...
SIDO Moro yang'ara nao, ikionyesha kundi njia, hata wakasimama na miradi uchumi




Ukurasa 13

Hoja ya Lema kuhusu bodaboda isigeuke kuwa malumbano kisiasa

BUFE
IJUMAA MACHI 10, 2023
Nipashe



Ukurasa 14

**JOTO WIKI WANAWAKE..., Lilian Kawa; 'jembe' la benki kutwaa tuzo za umahiri Afrika**

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA...

# Ziara zake 'zajibu', wawekezaji 270 wa EU waja nchini kujadili biashara, miradi

- Waingia mikataba zaidi Sh. trilioni moja
- Benki iliyoondoka miaka 16, yarejea



Rais wa Zanzibar Dk.Hussein Ali Mwinyi, katika hotuba ya kufunga Kongamano la Uwekezaji na Biashara kati ya Tanzania na Nchi za Umoja wa Ulaya, lililofanyika katika ukumbi wa Mikutano wa Kimataifa wa Julius Nyerere Jijini Dar es Salaam, tarehe 24, mwezi uliopita. **PICHA: IKULU SMZ.**

**Na Romana Mallya**

ILIKUWA tarehe 23 ya mwezi uliopita jijini Dar es Salaam, kulifanyika kongamano kubwa la kihistoria na la Biashara Kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU), likijumuisha washiriki 800, humo kukawapo wawekezaji 270 kutoka nchi 27 za EU.

Mafanikio ya kongamano hilo yakaainishwa na sehemu kubwa ya hadhira washiriki kuwa yamechangiwa na ziara ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alizozifanya katika nchi za Umoja wa Ulaya zilizokuwa na lengo la kuifungua Tanzania katika uchumi wa dunia.

Msingi wake ukaanikwa kwenye matendo, kauli, na uamuzi anaoufanya Rais Dk.Samia katika miaka miwili ya uongozi wake.

Kwa kurejea, hata pale alipopewa tu funguo za kuongoza nchi, alizuru nchi kadhaa duniani, zikiwamo za Ulaya, Asia na Afrika.

Rais Dk. Samia amekuwa akitolea ufafanuzi kwamba ni dhamira ya kufungua fursa za uwekezaji mitaji, masoko ya biashara na diplomasia uchumi, akitangaza uhalisia wa nchi na vivutio vyake, vikiwamo vya utalii.

Ni wastani wa wiki mbili sasa, Rais Dk. Samia akaweka mkazo kwa anacholenga, alipohamisha jukumu la uwekezaji kutoka Wizara ya Viwanda na Biashara, kuhamishia Ikulu.

Uhusiano wa alichokifanya Rais Dk. Samia, unapatiwa sehemu ya majibu kutoka kongamano la kimataifa jijini Dar es Salaam, kasi ya uwekezaji kimataifa na biashara nchini inashuhudiwa moja kwa moja ndani ya miaka miaka miwili ya utawala wa Rais huyo mwanamama.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dk. Hashil Abdallah, anaueleza mkusanyiko huo wa siku mbili, kwamba ni matokeo ya ziara yake Rais Dk. Samia alizofanya katika nchi za EU, kwa lengo la kuifungua Tanzania katika uchumi wa dunia.

Makamu wa Rais wa Benki ya Uwekezaji ya Umoja wa Ulaya (EIB), Thomas Ostros, akaweka wazi sababu za kurejea Tanzania baada ya kutokuwapo kwa miaka saba, ni kuridhishwa na maboresho ya mazingira mazuri ya biashara yaliyofanywa na Rais Samia.

Pia, bosi huyo wa EIB, akataja sababu nyingine ya kurudi nchini ni baada ya UVIKO- 19 kufifia nchini, hapo nyuma ya pazia kukionekana juhudi za Rais Dk. Samia.

**KILICHOJIRI MKUTANONI**

Kwenye kongamano la Dar es Salaam ilikuwa fursa ya mjadala wa kibiashara kimataifa, wawekezaji wa EU na wafanyabiashara wazawa. Wageni hao hata walipoondoka, wote kwa pamoja wakaonyesha nia ya kurejea nchini katika sekta tofauti.

Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, msomi wa uchumi, akamwakilisha Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kwenye hafla ya ufunguzi wa kongamano na likafungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi. Hapo pakashuhudiwa utiaji saini mikataba saba ya thamani zaidi ya Euro bilioni moja.

Kisekta, mikataba ikahusu huduma za Usafiri wa Anga, iliyosainiwa na Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi Prof. Makame Mbarawa, pia Waziri wa Mambo ya Nje, Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht.

Lengo lake ni kuongeza safari za ndege za moja kwa moja kutoka Dar es Salaam kwenda Kisiwa cha Mayotte, Ufaransa, ifikapo mwezi Juni, mwaka huu.

Mikataba mingine ni kati ya Bandari ya Antwerp-Bruges International na Mamlaka ya Bandari ya Tanzania, itakayoongeza usimamizi na kuimarisha miundombinu, ikiwamo bandari kavu na za maziwani, kuziongezea uwezo na ufanisi.

Pia, kukawapo hati ya makubaliano zinazohusu ujenzi wa Mradi wa Uzalishaji wa Umeme wa Kakono Hydro Power, mkoani Kagera uliofadhiliwa na Benki ya Maendeleo Afrika, chini ya ufadhili wa EU.

Vilevile, kukawapo mkataba uliotiwa saini baina ya Benki za Umoja wa Ulaya na Benki za Tanzania (EIB, CRDB, NMB na KCB) unaoruhusu uwekezaji mkubwa wenye thamani ya Euro milioni 540 (Sh1.333 trilioni).

Fedha hizo zinatolewa kwa lengo la kuwawezesha wawekezaji na wafanyabiashara, wakiwamo wanawake na sekta kama maji, utalii na kampuni zinazojihusisha na uchumi wa buluu.

Waziri wa Viwanda na Biashara, Dk. Ashantu Kijaji akawashawishi wanakongamano, kwamba kuna nchini ya soko la

INAENDELEA UK.14

UCHUMI

## KINAMAMA WANAPOJIVUNIA WIKI YAO...

# SIDO Moro yang'ara nao, ikionyesha kundi njia, hata wakasimama na miradi uchumi

**Na Christina Haule, Morogoro**

KAMPENI ya kinamama kupiga hatua kiuchumi inaendelea kote nchini, moyoni wakitawaliwa na falsafa 'kinamama wanaweza.'

Sasa hoja iliyo mbele yao wanashauriwa kupata elimu kwanza kabla ya kuanza biashara ya aina yoyote, ili kuwafanya waimarike na kuimarisha biashara zao, kwa kuona faida kwa wakati unaopaswa.

Meneja wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO) mkoa wa Morogoro, Joan Nangawe, anasema katika kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, wanawake wanapaswa kubadilika, kwa sababu kuna wanaoingia bila kujiandaa, wanaishia kukwama.

Zao la kutofuata nyendo hizo mara nyingi ni kufilisika mtaji wa mradi, sababu kubwa ni kukosekana elimu zinazotolewa kwenye ofisi za SIDO, zote nchini.

Meneja Nangawe anasema, kuna wanawake wengi wanaendesha ujasiriamali, lakini asilimia ndogo pekee ndio waliopata mafunzo hata kuweza kuwa na biashara endelevu.

Anasema wawekezaji wasiopata mafunzo wamekuwa wakijiingiza kwenye mikopo na wanaishia kushindwa kulipa kwa wakati.



Kinamama wajasiriamali wa mpunga, wakiwa katika mafunzo ya kuongeza thamani ya zao hilo, chini ya Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) mkoa wa Morogoro. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Nangawe anasema jumla kuna wanawake kati ya 950 na 1000 waliopatiwa mafunzo ya ujasiriamali kutoka kwa walimu kadhaa kupitia SIDO mkoani Morogoro, kati ya mwaka 2021 na sasa.

Anaainisha ni mafunzo yanayowagusa vijana na wanawake wa Morogoro vijijini na mjini, pia wilaya za Kilosa, Gairo, Kilombero na Malinyi. Ni mradi mahsusi kwa wanawake vijana, uliowezeshwa na taasisi ya CAMFED.

**MATUNDA YAKE**

Nangawe anataja zao lake ni vijana wamewezeshwa kiujuzi, kwenye maeneo ya uongezaji thamani mazao ya kilimo kama michikichi, kutengeneza sabuni mbalimbali, mpunga, mchele geto na viungo.

Maeneo mengine anayataja ni kuongeza thamani mazao viungo kama kutengeneza chaki, kusindika mafuta alizeti, pia kuzifungasha. Vilevile kuna ujuzi wa kutengeneza bidhaa; batiki, sabuni, kuandika kwenye fulana.

Anasema katika kufanikisha hayo, viwanda vidogo vya wanawake vimeanzishwa vikidhamiriwa kuwa endelevu kuwasaidia vijana wa kike wajifunze zaidi kupitia SIDO, huku wakiwezeshwa kupata mashine za kufanyia kazi, vifungashio na lebo.

Vilevile anarejea, kati ya miaka 2021/22, wamewezesha kufanya kazi na mradi, jumla ya vijana 50 waliopata mimba shuleni walifundishwa namna bora ya kutunza mazao kabla ya kutoka shambani na kabla ya kuyapeleka sokoni.

Hapo, inaelezwa wakasaidiwa kwa kuwatengenezea majokofu ya asili katika maeneo ya Doma na Dumila, ili yawasadie kutunza mazao yao, wakati wanapowasubiri wateja kwa bei, hata wakajikomboa kupitia shughuli zao.

Nagawe anasema, wamewafundisha namna ya kuongeza thamani ya mboga na matunda, hapo kukitajwa bidhaa; nyanya, karoti na vitunguu, vilevile wamejifunza kutengeneza juisi, piko mbalimbali, jamu na ukaushaji mboga na matunda.

Hivyo anasema, wanaendelea kuwafuatilia vijana hao kuona namna wanasimamia miradi wenyewe, kwa sababu bado wana mahitaji makubwa sokoni na ili wazalisha vilivyo, wanahitaji kupata sehemu rasmi za kuzalisha ambazo SIDO wana uwezo wa kuwapatia.

Anaeleza katika mwaka wa fedha uliopita, wamefanya mradi kwa kushirikiana na taasisi ya SNV, wakiwafundisha vijana wa jinsia zote kazi za saluni, urembo, biashara, lishe, kupamba ukumbi na ushonaji nguo, matarajio yaliyoko ni kushuhudiwa mabadiliko ya kijamii na taifa kwa ujumla.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, mpaka sasa wameshapatiwa jumla ya viwanda vidogo vitano, wanawake wakipatiwa mafunzo. Hapo anataja wilayani Ifakara, wamepatiwa mashine za usindikaji mafuta ya mawese, viungo na kiwanda cha kutengeneza chaki.

Meneja Nagawe anataja wilayani Malinyi, wamewawezesha kiwanda cha kutengeneza mafuta ya mawese ya kula, pia na ya kutengeneza sabuni.

Pia, kilichofanyika Morogoro Vijijini, anaainisha ni kwa vijana kutengeneza mchele unaoongezwa thamani, pia sabuni katika sura tofauti.

Katika maeneo ya Kilosa, Nagawe anasimulia kada hiyo ya umma; kinamama na vijana wamefundishwa utengenezaji na kuboresha thamani ya mazao; mchele na batiki, hali kadhalika wilayani Gairo, imefanyika kazi ya kuweka maandishi kwenye fulana; usindikaji mafuta ya alizeti na kuongeza thamani mazao ya mpunga.

Pia, kuna hatua ya ujumla, Nangawe anaeleza kwamba kuna vijana 20 wamepatiwa elimu na mashine za kushona nguo, kupitia mradi wa SNV na kwamba, inaendana na kupatiwa ujuzi wa kutengeneza keki.

**DIRA WANAYOPEWA**

Meneja huyo anatoa rai kwa wanawake kuacha tabia ya kukaa nyumbani pasipo kujishughulisha, ikianzia na kufika kwenye ofisi za SIDO kupata elimu za shughuli za kiuchumi na ujasiriamali, mahali waliko.

Nangawe anasema, kwa sasa wanaendelea kutoa mikopo kwa wajasiriamali na hata kwenye viwanda vidogo, ikigusa bidhaa za uzalishaji, pia kuhifadhi na kutunza kumbukumbu zao za biashara.

Anawakumbusha kinamama wanaoogopa kufanya biashara, wabadilike kwa kufanya biashara, huku wakizingatia miiko yake, ili kufikia faida wanayokusudia.

"Kikubwa, hatupaswi kuogopa ila tunapaswa kuelewa, kwa sababu, ili upate maendeleo kukopa inabidi tusikwepe, lakini unakopa kwa ajili ya nini na utalipaje unapaswa kujua,"anaeleza na kuendelea:

"Unakuta wengi hawaelewi na hawaifahamu biashara yao vizuri na kuogopa kuchukua pesa watakayoshindwa kuirejesha pengine."

Pia, anataja kuna kada ya wanawake wanaohofia kukopa, kutokana na kuwa na aina tofauti za ndugu au waume wasiotoa ushirikiano katika kile wanachofanya na hata hatari ya hela ya mkopo kuchukuliwa na mwanaume, au ikaingizwa kwenye masuala tofauti ya familia, pasipo kujali namna ya kurejeshwa.

Katika mustakabali huo, anawapa rai wanawake wajasiriamali kuhakikisha wanaangalia na kutathmini biashara zao kwa muda na wanaporidhishwa na manufaa tarajiwa, ndio wajiingize katika mikopo tajwa, badala ya kukimbilia hata ikawahatarishia maisha na kuwa mwiba kwao.

"Biashara nyingi za wajasiriamali zinakuwa za kwanza kufa, kwa sababu ya kukosa elimu. Mwingine anaanzisha biashara miezi sita tu, anakopa biashara inakufa.

"Nawashauri wanawake kupata elimu juu ya kile unachokifanya, hata kama unazalisha maandazi, lazima upate elimu kwa sababu kujua kuzalisha sio kujua biashara.

"Lazima uende kupata elimu, wataalamu wakuelekeze, uzalishe kiasi gani na kwa muda gani, faida itaanza kujitengeneza ndipo utaanza kukopa na kujizalishia ulipopungukiwa na uzalishaji ukiwa mkubwa utakuwa na kiasi cha kuweka kama faida, na kurejesha marejesho kwenye mkopo ulipochukua" anasema kitaalamu Nangawe.

**SAFARI WALIYOPITIA**

Anasema katika mwaka wa fedha 2021/22, wametoa mikopo 346, kati yao wanawake wakipata mikopo 175 yenye thamani ya shilingi milioni 172 na kati yake asilimia 95 zilirejeshwa.

Nagawe akirejea nafsi yake akiwa mwanamama, anasema ameweza kuwasaidia wanajinsia wenzake kuinuka kiuchumi, kupitia mafunzo mbalimbali waliyotoa SIDO katika maeneo mengi, hata akashuhudia wanawake wakijiamini na kutiwa moyo wa kuweza kufanya wanachodhamiria.

"Nimeona wanawake wengi wakija wamekata tamaa kabisa na hawajui nini wanaweza kufanya, lakini chini ya usimamizi wa SIDO, wanainuka licha ya kukatishwa tamaa kwenye eneo la familia. Pia nasi huwatia moyo na kuendelea kufanya biashara" anaeleza.

Meneja huyo anatumia hoja kielelezi ya kujifunza kwa kurejea nafsi na ujuzi wake, kwa manufaa ya kinamama anaowafunza, akijivuinia kwamba alipofikia SIDO amejifunza mengi hata nje ya taaluma iliyolengwa, akabahatika kutembelea maeneo mbalimbali ma kubadilishana uzoefu wa namna tofauti.

Anasema ameanza SIDO akiwa Ofisa Uendelezaji Teknolojia ya Chakula Daraja la Pili na sasa alikofika ni Meneja, hivyo anawataka wanawake wenzake kutokata tamaa, kwani changamoto hazikwepeki, ni sehemu ya maisha yake ya kila siku.

Hapo anaungwa mkono na mwanamke mjasiriamali na Mkurugenzi wa kampuni ya Kuzalisha Bidhaa za Kusindika, ikiwamo sabuni (Youth Soap and Supply) Susan Urio, anayesema amefaidika kupitia SIDO, baada ya kupata ujuzi wa kutengeneza bidhaa na kuanzisha kampuni inayomsaidia kwa sasa.


Hivyo, anawaasa wanawake kujiajiri kwa sababu inawezekana wakaacha kuwa wategemezi, kama watapatumia SIDO na kupata ujuzi stahiki wakajitengenezea fursa za kibiashara.

Kwa mujibu wa Kituo cha Taifa cha Takwimu nchini, takwimu za usawa wa kijinsia katika ajira, zinaonyesha bado hakuna mabadiliko makubwa ya mgawanyo wa ajira kisekta kwa kutumia tafsiri ya kitaifa kati ya mwaka 2014 na 2020/21, japokuwa ajira za serikali kuu na serikali za mitaa hazijatanuka sana.




Wanawake mkoani Morogoro, wanaoungana chini ya kivuli cha Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), katika hafla inayowahusu.

TAFAKURI YA MLALAHOI




## Hoja ya Lema kuhusu bodaboda isigeuke kuwa malumbano kisiasa



**NA JOSEPH KULANGWA**
+255 713 410008
(kulangwasos@gmail.com)

UVUTAJI sigara ni tabia iliyojengeka miongoni mwa watu duniani na Tanzania haijaachwa katika hilo, ingawa pia ni tabia inayopigwa vita kuwa ina hasara kiafya.

Wataalamu wa tiba wanasema uvutaji sigara unaathiri afya ya mwili na kusababisha matatizo mengi, ikiwamo pia kupoteza maisha kutokana na kuathiriwa vibaya na sigara.

Imefika hatua kuwa mtu aliye jirani na mvutaji yuko katika hatari kubwa ya kuathiriwa na moshi wa sigara inayovutwa na mwingine, hivyo kutakiwa kujiepusha.

Pamoja na hali kuwa hivyo na sigara kupigwa vita kiasi hicho, lakini upande mwingine wa sarafu unaonyesha kuwa sigara ni biashara nzuri inayotoa mchango mkubwa kwa uchumi wa nchi.

Ndiyo sababu kuna viwanda vya sigara, pia kuna wakulima wa tumbaku, ambayo ni malighafi ya sigara na wamekuwa wakisaidiwa kwa mbolea na pembejeo zingine, ili kuzalisha kwa wingi na kulisha viwanda.

Hivyo sigara ni hatari kwa maisha ya binadamu, ina faida pia kwa maisha yao, kupitia viwanda vinavyozalisha bidhaa hiyo na kutoa ajira, vilevile kuchangia pato la taifa.

Kama tunakubaliana katika hili, basi tutafakari pia katika kauli ya Mjumbe wa Kamati Kuu ya Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), mbunge wa zamani wa Arusha Mjini, Godbless Lema.

Lema aliyekuwa uhamishoni nchini Canada kisiasa, alirejea hivi karibuni nchini na kupokewa na umati wa wafuasi wa chama chake, wakiwamo madereva wa bodaboda katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), wakafuatana mpaka jijini Arusha.

Wakati wote wakifurahia mapokezi hayo, kumbe yeye moyoni alikuwa akisononeka, kuwaona wafuasi wake watumia bodaboda wakiteseka, licha ya wao kufurahia ujio wa kiongozi wao. Hakuzuia hisia zake, akasema:

"Bodaboda, wakati ninyi mnanipokea kwa shangwe, mimi nilikuwa na huzunika. Bodaboda si a ira, ni umasikin iunaopitiliza. Hiyo ni ajira ya laana, ikemeeni. Hamuwezi kufanya ajira kwa kukimbiza upepo. Sh 7,000 kwa siku! Hapana!"

Alipoisikia kauli hiyo, Mbunge wa Singida Magharibi, Elibariki Kingu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), akaibuka na kumpinga Lema kwa maneno yake akifafanua kuhusu bodaboda.

Akasema: "Kuna nchi nyingi zinaongoza kwa kuwa na waendesha bodaboda. Hii ni kazi ya heshima na inarahisisha usafiri wa watu kujenga uchumi wa nchi.

"Kitendo cha mwanasiasa huyo kuwatukana bodaboda katika taifa letu kwamba wamelaaniwa, hatuwezi kuacha bila ya kujibiwa kwenye majukwaa ya kisiasa."

Akasema kuwa CCM inawaheshimu na itawasaidia kwa kuanzisha mikakati ya kuchochea maendeleo yao kiuchumi.

Hizo ndizo siasa za nchini. Tayari suala muhimu na nyeti kama hilo limehamia kwenye majukwaa, badala ya kutafakari hoja kwa uzito wake.

Ili kuongeza uzito wa hoja yake, Lema alipomsikia, Kingu akaona aje na lingine akiwaambia, bodaboda hawana bima kama ilivyo kwa magari, hivyo wapatapo ajali hawalipwi chochote zaidi ya kuishia kupata ulemavu wa kudumu.

Nadhani Lema hakuwa na nia ya kuwatukana, kama inavyoonekana, lakini alikuwa akihadharisha kutoka na na madhila wanayoyapata vijana hao yakiwamo ya magonjwa yatokanayo na upepo na baridi kama vile baridi yabisi.

Madhila kama ya ajali, katika hospitali nyingi hivi sasa kuna wodi maalumu za madereva hao ambao kila siku wanapata ajali barabarani na kuishia kupoteza maisha au kukatwa baadhi ya viungo.

Ninavyohisi Lema katamka kwa kuwapenda vijana wake na ndiyo sababu akaamua kufunguka kuwatetea kwa njia hiyo. Hakuna asiyewatambua kuwa ni Watazania wanaojitafutia. Hata Rais Samia Suluhu Hassan amelisema hilo hadharani.

Maoni yangu mojawapo, kurahisisha huduma hizo za usafiri, bora kuhalalisha za miguu mitatu kuliko miwili, ikishindikana tuhakikishe wana bima, lakini pia wanasimamiwa kuheshimu sheria za barabarani na si kuwadekeza kwa kuwapunguzia faini ili waendelee kuvunja sheria.

Inafaa tukapunguze siasa kwenye maswali magumu. Alamsiki!

UCHUMI

## KINAMAMA WANAPOJIVUNIA WIKI YAO...

# Lilian Kawa; 'jembe' la benki kutwaa tuzo ya umahiri Afrika

**Na Mary Kadoke**

**SWALI:** Lilian Kawa, ningependa kufahamu historia yako kwa kifupi, ikiwamo taaluma na uzoefu wako katika utendaji ndani ya sekta ya fedha na benki?.

**JIBU:** Mimi ni mke, binti, dada, shangazi na rafiki. Nilianza kazi katika sekta ya fedha, takribani miaka 14 iliyopita, kama karani katika tawi mojawapo la benki kongwe nchini.

Sikuwahi kuwaza au kutegemea kama nitafanya kazi katika sekta ya fedha; bali nilikuwa na mipango mingine tofauti. Hadi sasa nimefanya kazi katika benki nne tofauti na nimekuwa nikipanda vyeo taratibu, kutokana na kujiongeza katika elimu na jitihada katika utendaji wa kazi.

**SWALI:** Ukiwa mtaalamu na mzoefu katika idara ya 'compliance'... inapotamkwa neno 'compliance' katika benki, ina maana gani?

**JIBU:** 'Compliance' ni neno geni lisilokuwa na tafsiri ya moja kwa moja. 'Compliance' inamaanisha miongozo na taratibu kwa kila mfanyakazi, idara mbalimbali na taasisi kwa ujumla, katika kuhakikisha kuwa, sheria za nchi, sheria zinazoongoza sekta ya fedha (ndani na nje ya nchi) zinafuatwa, ili kujenga dhana ya uadilifu na utawala bora katika kuendesha biashara ya benki, kuzuia upotevu wa fedha za wawekezaji na amana za wateja na kuhakikisha benki inapata faida stahiki katika biashara yake.



Lilian Kawa. **PICHA: MARY KADOKE**.

**SWALI:** Unapoelekea kupata tuzo ya 'Women In Management Awards Africa (WIMA), hii kwako ina maana gani?

**JIBU:** Ni kweli kwamba ni mmoja wa washindi wa tuzo ya Women In Management Awards Africa (WIMA) 2023. Tuzo hii inadhihirisha jitihada zangu katika kuongoza na kusimamia masuala ya 'compliance' pamoja na kushirikiana na viongozi wenzangu ndani Diamond Trust Bank

(T) PLC zimeonekana. Tuzo hii ni alama ya kuonyesha kuwa lolote linawezekana kwa jitihada thabiti.

Ni kweli kwamba taaluma hii ndani ya benki nyingi zinaendeshwa na wanaume. Tuzo hii iwe chachu pia kwa wanawake wenzangu walio na nia ya kujiendeleza kwenye 'compliance' kwamba inawezekana na wasikate tamaa.

SWALI: Una ushauri gani kwa wengine wote ndani na nje ya benki yako kufikisha kiwango cha mafanikio kama uliyoyapata?

**JIBU:** Mungu ni wetu sote. Ni vyema kumtegemea muumba wetu bila ya kusahau jitihada binafsi katika kazi. Ningependa kuwatia moyo mabinti na wanawake wenzangu kujiamini, katika kupata maendeleo mengi zaidi.

Ni vyema kuelewa kwamba, mafanikio yanaanza na ushindani binafsi wa kupiga hatua mmoja mmoja hadi kufikia malengo yetu ya maisha.

**SWALI:** Ni changamoto gani unazokutana nazo kama mkuu wa idara na mwanamke katika utendaji kazi kila siku?

**JIBU:** Ukweli usiofichika, ni kwamba taaluma hii inaongozwa na wanaume kwa wingi, kama ilivyo tu taaluma zingine katika sekta ya fedha. Hii

inamaanisha kwamba, mwanamke yeyote anayetaka kujenga taaluma katika 'compliance' lazima atalazimika kuweka jitihada za ziada; kwanza kuwashinda wanaume waliopo katika tasnia na kisha kujiamini.

Kuonyesha uwezo katika kazi na kujiendeleza kila mara ni mbinu nilizojiwekea kama nguzo katika kazi yangu. Ni kweli kwamba, wanawake ni

wachache sana kwenye taaluma hii, lakini inabidi tuanze kupenya na kuonyesha uwezo wetu.

Ningependa kuwatia moyo wanawake wenzangu hasa wakati huu tunapoadhimisha siku ya wanawake duniani, kuj amini katika uwezo wa

kitaaluma tulio nao, kwani ndio ushindi wetu dhidi ya mfumo dume.

**SWALI;** Mtazamo uliopo juu ya idara ya 'Compliance' ni kwamba ipo kuzuia biashara ndani ya benki? Je, wana uelewa wa kutosha kwamba mpo kwa ajili ya kuhakikisha benki inafuata taratibu na sheria zilizowekwa kusimamia sekta ya fedha?

**JIBU:** Safari bado ni ndefu, ila imeshaanza kwa njia sahihi. Napenda sana kutoa elimu ya 'compliance' kwa namna ambavyo mtu atawaza mchango wake ni upi katika kukuza ustawi au kuzamisha benki au taasisi.

'Compliance' ni kitengo ambacho kinahakikisha kuwa jina la taasisi linabaki kuheshimiwa kutokana na kuheshimu na kufuata sheria, hivyo kupelekea upatikanaji wa mazingira bora ya kufanya biashara na hatimaye faida kwa benki au taasisi.

Madhara yatokanayo kwa kupuuzia 'compliance' ni pamoja na taasisi kufutiwa leseni ya biashara na mamlaka stahiki; taasisi kupewa adhabu ya kulipa fedha; mkuu wa taasisi au mfanyakazi kupewa adhabu ya kulipa fedha; kifungo jela au kufukuzwa kazi.

Taasisi husika kukosa jina zuri kwenye soko na hatimaye kukosa, hata wateja na biashara

Madhara yatokanayo na kutozingatia 'compliance' ni makubwa sana na yanatishia uwapo wa taasisi au benki, ni dhahiri kamwe hayawezi kupuuzwa.

Pia inaonyesha kwamba bila 'compliance'. Hakuna biashara endelevu au uhakika wa taasisi kuwepo kwenye biashara.

Kwa mantiki hii, 'compliance' ipo kwa nia ya kuhakikisha kuwa biashara inafanyika katika mazingira yaliyosahihi na inayozingatia sheria za nchi.

# ZIARA ZAKE 'ZAJIBU', WAWEKEZAJI 270 WA EU WAJA NCHINI KUJADILI BIASHARA, MIRADI

**INATOKA UK.11**

nchi za EU lenye zaidi ya watu milioni 400.

**DK. MPANGO AFUNGUKA**

Akifungua kongamano hilo, Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango anawataka wawekezaji kufika kwenye maeneo yanayoendana na mahitaji, lengo ni kuiwezesha Tanzania kufikia penye Dira ya Taifa ya 2025; uchumi uliopo kupiga hatua zaidi.

Mchumi Dk. Mpango, anataja vipaumbele vya nchi ni, uwekezaji katika kilimo, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya kilimo, viwanda vya dawa na vifaa tiba, ujenzi, sayansi, teknolojia na maendeleo ya viwanda katika kizazi cha nne. Anasema, serikali imedhamiria kuboresha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara, kwa kuendelea kurekebisha sheria. Hapo inahusu kuboresha mifumo ya ulipaji kodi na sera zake kwa nchi 10.

Zingine zinatajwa ni kuimarisha Kituo cha Uwekezaji Tanzania (TIC), ambacho sasa kiko chini ya Ofisi ya Rais, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA).

Mengine. Dk. Mpango anayataja ni kupatika umeme, uendelezaji bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na Bandari Kavu ya Kwala.

Vilevile anataja ni kujenga barabara na reli, kasha kuanzishwa wa Sheria ya Uwekezaji ya 2022, ikifuta ya awali, mwaka 1997.

**VIONGOZI WA EU**

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Manfredo Fanti, anaeleza kufurahishwa na majadiliano yaliyofanyika kati ya Tanzania na wawekezaji wa EU, kwamba yameiongezea Tanzania fursa za uwekezaji.

Fanti anasema kupitia kongamano hilo wawekezaji wa EU waliofika Tanzania baadhi wameonyesha nia ya kurejea mapema kwa ajili ya kuendeleza mazungumzo yanayohusu uwekezaji katika sekta mbalimbali.

Waziri wa Biashara na Vivutio vya Uchumi wa Ufaransa, Olivier Becht, anaibainisha nia ya Ufaransa ya kuimarisha uwekezaji Tanzania, hasa katika sekta za kimkakati, akinena ushirikiano baina ya nchi hizo ni wenye, kutokana na hali ya Tanzania kuwa nchi inayokua kwa haraka kiuchumi sasa.

**VIONGOZI WA TANZANIA**

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashantu Kijaji, anafafanua kwamba soko la nchi za EU lina zaidi ya watu milioni 400.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, anawaeleza wageni hao fursa za kuwekeza kwenye sekta kama za; kilimo uchumi wa bluu, nishati mbadala, viwanda, madini, mafuta na gesi, ujenzi, usafiri na usafirishaji na huduma za kifedha zinazopatikana Tanzania Bara na visiwani Zanzibar.

Anawaeleza dira ya serikali ya Rais Dk. Samia, ni kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, zichangamke na kuchangia kasi ya maendeleo ya uchumi na jamii.

"EU inaipatia Tanzania ruzuku ya Euro milioni 23 (Sh. bilioni 56.98) kusaidia utekelezaji programu za uboreshaji wa mazingira ya uwekezaji na biashara (blue print) pamoja na kuboresha kazi ya udhibiti wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS)," anafafanua Dk. Mwinyi, akiahidi TBS itahakikisha bidhaa zinazozalishwa nchini zinakidhi viwango vya ubora kimataifa, hata kurahisisha kufikia masoko ya kimataifa ya EU.

**FURSA ZANZIBAR**

Katibu Mkuu, Uchumi na Uwekezaji - Ofisi ya Rais Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Dk. Habiba Hassan Omar, anaeleza namna serikali ya Zanzibar, inavyoboresha mazingira ya biashara na uwekezaji, ikiimarisha Sheria ya Biashara iliyofanyiwa marekebisho.

Anaorodhesha maeneo ya uwekezaji visiwani ni: Uvuvi wa Bahari Kuu; Kuvuna Mwani; Majongoo Bahari; Utalii wa Bahari; na Ujenzi wa Nyumba za Makazi za Bei Nafuu, lengo kupunguza ujenzi holela mijini visiwani.



## CBE yazindua programu kuwajenga wanafunzi kuwa wabunifu

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

CHUO cha Elimu na Biashara Dodoma (CBE) kimezindua programu atamizi za biashara na tekolojia na klabu za ujasiriamali kwa shule za sekondari ili kuwajengea uwezo wanafunzi kuwa wabunifu.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Edda Luoga, alibainisha hayo jana wakati wa uzinduzi wa programu hiyo uliofanyika Kampasi ya Dodoma.

Alisema mafunzo hayo yatafundishwa kwa ushirikiano na Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) malengo yakiwa ni kuwafanya wanafunzi kuwa na chachu ya kujifunza ujasiriamali wakiwa bado shuleni.

Alisema malengo ni kuunga juhudi za serikali katika kulea ndoto za wanafunzi wabunifu ambao watajifunza elimu ya biashara ya masomo ya uchumi na utunzaji wa kumbukumbu na fedha.

"Hivyo mafunzo hayo yatawasaidia kuanzisha ujasiriamali na kuwezesha kuchangia pato la taifa na serikali kuipeleka Tanzania uchumi wa kati.

"Tupo hapa kwa ajili ya kulea mawazo ya wanafunzi wabunifu ili waweze kufanya biashara kamili wakiwa hapa chuoni na hatimaye wajiajiri wenyewe," alisema.

Mratibu wa programu hiyo, Adrian Ndunguru, alisema kwa mwaka 2023 watazifikia shule sita ambazo kila moja kuna wanafunzi 400, kwamba watakaofikiwa ni 2,400.

Hivyo aliwataka wanafunzi wenye ubunifu kujiunga na kujisajili ili kujifunza ujasiriamali na waweze kuwa wafanyabiashara wakubwa watakaowezesha kuongeza uchumi wa Taifa.

Akizindua programu hiyo, Mkuu wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri, aliwataka wanafunzi wote kusoma kwa bidii ili waweze kujitengenezea maisha yao ya badaye yatakayo wawezesha kujiajiri.

Pia aliwataka vijana kutokubali kutumiwa na watu wasiolitakia mema taifa kwa malengo ya kuvuruga amani iliyopo, badala yake wawe wa kwanza katika kutoa taarifa kwenye vyombo husika kuanzia ngazi ya chini.

# SMT, SMZ zashirikiana utatuzi sekta ya mifugo

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Mhina, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), zinashirikiana kutatua kero zilizoko katika sekta ya mifugo ili kufikia uzalishaji wenye tija.

Alibainisha hayo juzi wakati akifungua kikao cha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kilichofanyika mkoani hapo.

"Tumekuwa tukishirikiana pia kwenye maeneo ya masoko kuona ni namna gani tunaweza tukaimarisha masoko ya bidhaa za mifugo kwa pande zote mbili.

Kwa hiyo ushirikiano huu unalenga kuondoa vikwazo ambavyo vinaweza kuifanya biashara ya mifugo isikue kwa haraka," alisema Dk. Mhina.

Dk. Mhina alisema sehemu zote za bara na Zanzibar kuna viwanda vya kuzalisha bidhaa za mifugo ikiwamo nyama, ngozi, maziwa na bidhaa nyingine, hivyo ushirikiano huo utasaidia kuimarisha sekta ya mifugo.

Alisema ushirikiano huo umelenga kutatua kero kwenye maeneo mbalimbali hususani za kikodi kwa kushauri mamlaka husika ziweze kufanya marekebisho, ili kuwezesha biashara kufanyika kwa urahisi zaidi kati ya pande zote mbili za muungano.

Aidha, alibainisha kuwa ushirikiano huo utajikita katika maeneo ya utafiti na mafunzo ili waweze kujifunza kila upande ni namna gani sekta zinafanya ili kuzalisha kwa tija mifugo na bidhaa zake.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Dk. Omary Ali Amir, alisema wanatumia ushirikiano huo kujifunza tafiti mbalimbali na pia kujenga uwezo wa wataalamu wao kupitia Tanzania Bara kwa kuwa wako mbele kwenye masuala mengi ikiwamo uzalishaji, masoko na utafiti.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule (wa pili kulia), akikata utepe kuzindua kampeni ya mwanamke na Samia yenye lengo la kuchochea uchumi wa wanawake pamoja na kuelimisha vijana, uliofanyika wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani mjini Kondoa juzi. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wanawake REA watoa msaada mitungi ya gesi, majiko banifu

**Na Paul Mabeja,** BAHI

JUMUIYA ya wanawake wa Wakala wa Nishati Vijijini (REA) wamekabidhi misaada ya mitungi ya gesi na majiko banifu yanayotumia kuni na mkaa, ili kupunguza athari za uharibifu wa mazingira katika vijiji vya Zanka na Kigwe wilayani Bahi.

Msaada huo ulikabidhiwa mbele ya Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule.

Akizungumza wakati wa makabidhiano hayo, Senyamule aliwapongeza wanawake hao kwa kuonyesha kuwajali wanawake wenzao pamoja na kutunza mazingira.

"Leo tupo na REA tumeshuhudia namna bora walivyoamua kuadhimisha siku hii, jamani hongereni sana mmeamua kushiriki kwa upendo mkubwa sana,"alisema Senyamule.

Aidha, alisema wanawake wanapata athari nyingi kwa kutumia kuni mojawapo ni magonjwa ya macho na kifua, hivyo kujikuta wakishindwa kuendelea na uzalishaji. "Sisi Tanzania tunajivunia sana kwa kuwa na kiongozi mkuu mwanamke imara, jasiri, mchapakazi (Samia Suluhu Hassan) ni mara ya kwanza kwa nchi yetu kupata kiongozi ambaye ni mwanamke,"alisema.

Kadhalika, alisema wanajivunia kazi ambayo anaifanya ikiwamo kuhakikisha wanawake wanaendelea kupata fursa mbalimbali.

Senyamule alisema serikali inaweka mikakati ya kuhakikisha inaulinda Msitu wa Chinene pamoja na kuwachukulia hatua wanaoharibu mazingira, kuandaa operesheni maalumu ya kuulinda msitu huo.

Mkurugenzi wa Uendelezaji Masoko na Teknolojia REA, Mhandisi Advera Mwijage, alisema wameamua kuwasaidia wakazi wa vijiji hivyo kutokana na umaskini uliopo katika maeneo hayo.

Alisema kinamama wengi wamekuwa wakijishughulisha na ujasiriamali, hivyo wanaamini watapata muda mwingi wa kufanya biashara kuliko awali walivyokuwa wakiutumia kutafuta kuni.





# Wanafunzi msingi, sekondari wapewa siri kufikia ndoto zao

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MWENYEKITI wa Mtandao wa Askari Polisi Wanawake Mkoa wa Mbeya, ACP Christina Musyani, amewataka wanafunzi wa shule za msingi na sekondari mkoani hapo kujitunza, kutoruhusu miili yao kutomaswa na mtu yeyote ili kujiepusha na vitendo vya ukatili wa kijinsia ambavyo vinaweza kukwamisha ndoto zao.

ACP Musyani alitoa kauli hiyo jana alipozungumza na Nipashe ikiwa ni siku moja tangu watoe misaada ya vitu mbalimbali kwa wanafunzi wa kike katika Shule ya Sekondari Kipoka, Shule ya Msingi Nyerere na Makongolosi.

ACP Musyani ambaye ni Ofisa Mnadhimu namba moja, Mkoa wa Mbeya, alisema watoto wa kike wanapaswa kupaza sauti zao kuhusu vitendo wanavyofanyiwa ikiwamo ulawiti, ubakaji na vipigo. "Nawaomba sana watoto wangu msikae kimya pindi mnapofanyiwa vitendo vya ukatili au uhalifu wa aina yoyote, mtoe taarifa kwa wazazi, walezi au walimu kwa ajili ya hatua zaidi za kisheria,"alisema ACP Musyani.

Aliupongeza uongozi wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Makongolosi kwa jitihada za kukabiliana na vitendo vya ukatili wa kijinsia, ikiwemo kuwachukulia hatua za kinidhamu wale wote wanaohusika na vitendo hivyo.

Diwani wa Kata ya Bwawani, Sairon Mbalawata alisema misaada waliyoitoa kwa watoto hao hususani taulo za kike zitasaidia kupunguza utoro kipindi cha hedhi na kuongeza bidii katika masomo.

Mkuu wa Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Simon Mayeka, aliwasisitiza wanawake wa wilaya hiyo, kuongeza umakini katika malezi ya watoto ili kuwaepusha na vitendo vinavyohatarisha usalama wao.

Hivyo, aliwashauri wazazi na walezi kuwatumia wasaidizi wa kisheria kuwashughulikia wale wote wanaohusika na vitendo hivyo sambamba na kuripoti kwa Jeshi la Polisi kuchukuliwa hatua.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera (wa pili kulia), akijadiliana jambo na Mkurugenzi wa Mradi wa Kibowavi kutoka Shirika la Helvetas Daniel Kalimbya (wa tatu kulia) na viongozi mbalimbali wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Rungwe juzi. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# SIDO kutengeneza mashine za kisasa ili kukuza uchumi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MENEJA wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo nchini (SIDO) mikoa ya Songwe na Mbeya, Henerick Mdede, amesema karakana ya shirika hilo imedhamiria kutengeneza mashine za kisasa kwa lengo la kukuza uchumi.

Akizungumza na Nipashe jana Mdede alisema wamejipanga kuhakikisha mwaka 2022 unakuwa wa mapinduzi kwa kuhakikisha sekta ya viwanda inakuwa na tija kwa wajasiriamali. "Miongoni mwa shughuli tunazokusudia kwa mwaka huu ni uanzishwaji wa viwanda vidogo katika ngazi ya mkoa ili kuhakikisha maendeleo ya teknolojia na huduma za ufundi zinazidi kushika kasi," alisema Mdede.

Alifafanua kuwa SIDO Mkoa wa Mbeya inamiliki karakana kubwa ambayo inabudi na kutengeneza mashine mbalimbali na kwamba kwa mwaka jana walifanikiwa kutengeneza 130 ambayo zilienda kusaidia kwenye uzalishaji wa bidhaa mbalimbali.

Kwa upande wake Mratibu wa karakana ya SIDO Mbeya, Mhandisi Cosmas Kinasa, alisema karakana inaendelea kubuni mashine mbalimbali na kwamba kwa sasa mashine 58 zipo sokoni ambazo zinaweza kuzalisha bidhaa mbalimbali.

Mhandisi Kinasa alisema mashine za kusaga unga zipo za aina mbili ambazo zinauzwa Sh. milioni 56 ambapo mahindi yanachakatwa kwa mtindo wa kisasa, kuna mashine za kuchakata mafuta ya alizeti.

Alisema mbali ya kutengeneza mashine SIDO hutoa mafunzo ya ujasiriamali na mikopo inayowawezesha wananchi kufikia azma ya serikali ya kuwa Tanzania ya viwanda kutokana na upatikanaji wa umeme vijijini.

Baadhi ya wajasiriamali jijini Mbeya waliiomba SIDO kuuza mashine za kuchakata mazao kwa bei nafuu ambayo wanaweza kuimudu kuliko ilivyo sasa ambapo huuzwa kwa bei kubwa.

# W'biashara soko la Forest walia ubovu miundombinu

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

WAFANYABIASHARA wa Soko la Forest jijini Mbeya, wameomba uongozi wa soko hilo kuwatengenezea na kuboresha miundombinu ili wafanye biashara katika mazingira mazuri.

Wakizungumza na Nipashe jana baadhi ya wafanyabiashara wa soko hilo walisema mvua zinazoendelea kunyesha zimeharibu miundombinu ya soko hilo na kusababisha wateja kutofika maeneo hayo.

Miongoni mwa wafanyabiashara hao, Ekinala Abbas, alisema kipindi cha mvua barabara ndani ya soko hilo hazipitiki hali inayosababisha wateja kushindwa kufika maeneo hayo hali inayosababisha ukata na bidhaa zao kuharibika.

Alisema licha ya miundombinu ya barabara kuharibiwa na mvua lakini soko hilo halina choo hali inayosababisha kutumia umbali mrefu kwenda kufuata huduma ya choo maeneo mengine.

"Serikali ilijenga soko hili muda mrefu sana lakini tatizo ni kwamba hakuna miundombinu rafiki kwa ajili ya kufanyia biashara zetu, wateja wanatukimbia kwa sababu ya mazingira na mbaya zaidi hatuna hata choo tunaomba mtusaidie," alisema Abbas.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Soko la Forest, Jackson Kamotola, alikiri kuwapo kwa ubovu wa miundombinu katika soko hilo na kwamba licha ya vizimba na majengo lakini hali ya biashara hairidhishi.

Alisema wajasiriamali na wateja siyo wengi kutokana na jiografia ya eneo hilo, hivyo wanaendelea kuiomba serikali kuboresha miundombinu ya majengo na vyoo ili kuwavutia wawekezaji na wateja.

Alisema licha ya ukongwe wa Soko la Forest lakini linakabiliwa na uhaba wa wafanyabiashara kutokana na miundombinu mibovu hivyo kukosa wateja.



# 'Wanawake wa Zanzibar mna fursa nyingi kuleta maendeleo'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, amesema wanawake wa Zanzibar wana fursa nyingi za kuleta maendeleo hasa kupitia sekta ya utalii.

Aliyasema hayo jana Zanzibar wakati wa hafla ya uzinduzi wa kitabu kiitwacho 'Nyayo za Wanawake wa Zanzibar' ambacho kimeeleza mchango wa wanawake katika maendeleo mbalimbali.

Alisema kitabu hicho kinatoa fundisho kuwa mafanikio huanza na ndoto zinazojenga malengo yanayolindwa na jitihada, hatimaye kufikia kileleni kwa kutumia ushirikiano pamoja na umoja.

Alisema kuna umuhimu wa kubadilisha matatizo kuwa fursa, kupambania wanachokiamini na kutovunjika moyo pamoja na kujitolea kwa ajili ya wenzao.

Alisema wanawake walioandikwa katika kitabu hicho wamepambana kuleta maendeleo na kuwa mfano kwa wanawake wengine.

Alisema Zanzibar kuna wanawake wengi ambao wana mchango mkubwa, wanahitaji kutambulika katika nyanja mbalimbali ikiwamo siasa, sanaa, michezo, biashara, kilimo na sayansi.

Hivyo, aliwataka wanawake wote wa Zanzibar kushiriki kikamilifu katika kujenga nchi kwa sababu mchango wao ni muhimu na kitabu hicho ni ushahidi kwa sababu michango ya wanawake imeelezwa katika sekta mbalimbali.

Mtunzi wa kitabu hicho, Hannah Mccarrrick, alisema lengo la kuandikwa kwa kitabu ni kuwaibua na kuwatangaza wanawake wa Zanzibar waliofanya mambo makubwa ya kimaendeleo ambao hawajatambulika.

Alisema wanawake hao ni mfano wa wanawake wengine na kitabu hicho kitakuwa ni mwendelezo wa kuwaibua na kuwatangaza wanawake wengine waliofanya mambo makubwa ya maendeleo katika jamii zao na nchi kwa ujumla.

Wakizungumza baada ya uzinduzi huo, wanawake walioandika simulizi zao katika kitabu hicho akiwamo Balozi Amina Salum Ali, alisema amefarajika kuwa miongoni mwa wanawake waliopata nafasi hiyo na kuwataka wanawake kuungana pamoja katika kutetea na kudai haki zao za msingi.




Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Halima Bulembo (katikati), akipokea misaada ya vyakula na mahitaji mengine ya kibinadamu vilivyotolewa na Benki ya Biashara Tanzania, mkoani Dar es Salaam kwa ajili ya kusaidia kituo cha kulelea watoto yatima cha Hisani Orphanage Kigamboni ikiwa ni utaratibu wa benki hiyo kusaidia jamii. Kutoka (kulia) ni Meneja wa benki hiyo, Tawi la Kigamboni, Lameck Buberwa, Meneja Mawasiliano na Uhusiano, Gloria Mutta na Ofisa Masoko, Dorothea Lyimo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAMWA yatoa elimu ya kujilinda na udhalilishaji

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIKA kuadhimisha Siku ya Wanawake Duniani, Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA-Zanzibar) kimetoa elimu kwa wanafunzi shuleni na kwenye madrasa.

Lengo la kutoa elimu hiyo ni kuwawezesha watoto kujitambua na kujilinda na udhalilishaji wa kijinsia.

Akizungumza jana baada ya utoaji elimu ya udhalilishaji kwa wanafunzi wa Shule ya Hasnuu Makame Mkoa wa Kusini Unguja, Ofisa Msimamizi wa kitengo cha kupinga vitendo vya udhalilishaji kutoka TAMWA Zanzibar, Zaina Salum Abdallah, alisema elimu hiyo itasaidia kupambana na vitendo vya udhalilishaji.

Alisema miongoni mwa maoni waliyoyapata kwa wanafunzi, walimu na jamii wakati wa utoaji wa huduma hiyo wanataka elimu ya udhalilishaji iwekwe katika mitaala ya elimu ili somo hilo kufundishwa kila siku shuleni.

Alisema kuongezeka kwa utandawazi ikiwamo matumizi ya mtandao kunasababisha kuongezeka kwa vitendo vya udhalilishaji, hivyo ni vyema jamii kuwalinda watoto na vitendo hivyo.

"Wengi tuliowafikia ni vijana na watoto, hivyo lengo letu ni kuona matukio haya ya udhalilishaji yanapungua au kuondoka kabisa lakini pia watoto na wasichana kujitambua,"alisema.

Wanafunzi wa Shule ya Hasnuu Makame Mkoa wa Kusini Unguja ambayo ni miongoni mwa shule iliyopatiwa elimu hiyo walisema wanafunzi wanapofanyiwa vitendo vya udhalilishaji hupata msongo wa mawazo na kutofanya vizuri katika mitihani yao shuleni.

Harouna Khamis Adamu ni miongoni mwa wanafunzi wa shule hiyo, aliiomba serikali ichukue hatua kali za kisheria kwa atakayethibitika ametiwa hatiyani kwa makosa ya udhalilishaji.

Shekha Nassor Said alisema kuwa elimu hiyo ya udhalilishaji ni vyema kutolewa mara kwa mara ili kuepukana na vishawishi vinavyopelekea kudhalilishwa.

Mwalimu Mkuu wa shule hiyo, Bakari Muhammed Ali, alisema elimu hiyo itaongeza kasi ya kupambana na vitendo hivyo.

"Shule yetu ni ya bweni na ina mchanganyiko wa wanafunzi wa kike na kiume, hivyo elimu ya udhalilishaji ni muhimu sana ili wanafunzi kuwa na uelewa," alisema.

Aidha, alivitaka vyombo vya sheria vinavyosimamia kesi hizo kuwa waadilifu na kuharakisha usikilizaji wa kesi hizo na hukumu itolewe kwa haraka.

## Dk. Mwinyi awafunda watendaji wakuu mashirika ya umma

**Na Mwandishi Wetu**

MASHIRIKA ya umma yametakiwa kujitathmini kwa kujipambanua na kufungua ukurasa mpya wa ufanisi na uendeshaji kwa kuacha utendaji wa kusuasua.

Pia wametakiwa kuja na mikakati ya mageuzi na kuleta mabadiliko ya haraka yenye kutoa huduma za uhakika kwa wananchi na tija kwa serikali.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, aliyasema hayo Ikulu Zanzibar, alipozungumza na watendaji wakuu wa mashirika hayo.

Dk. Mwinyi aliwaelekeza kufanya marekebisho na maboresho ya kiutendaji watakapoona mazingira hayapo sawa kwa mustakbali wa mashirika hayo na serikali kwa ujumla.

"Tunataka mashirika ya umma yaendane na kasi ya awamu ya nane kwa kufungua ukurasa mpya wa nidhamu, ukurasa wa kufanya kazi kwa bidii, ukurasa wakuleta faida na kubwa kuliko lote ni huduma za uhakika kwa wananchi," alisema Dk. Mwinyi.

Dk. Mwinyi aliyataka mashirika yanayotoa huduma kwa wananchi kutafuta ufumbuzi wa haraka kutatua matatizo yanayowakabili na kuzigeuza kuwa fursa zenye tija, kuleta mabadiliko chanya ikiwamo kubadili mifumo ya taasisi zao inapoonekana inafaa kwa maslahi ya umma. Akizungumzia Mamlaka ya Maji Zanzibar, (ZAWA) na Shirika la Umeme Zanzibar (ZECO) Rais Dk. Mwinyi alieleza ni mashirika yanayotoa huduma na kugusa maisha ya watu moja kwa moja na kueleza haitoshi kutoa huduma pekee bila ya kuingiza faida kwa ajili ya uendeshaji wa mashirika hayo.

Aidha, aliwashauri ZAWA kuacha kutumia pampu zinazotumia umeme wa ZECO badala yake watumie umeme wa jua ili kukwepa matatizo ya kuungua kila mara na kuwaondolea wananchi shida ya kukosa maji kila wakati.

Akizungumzia baadhi ya Mashirika ya Umma yanayosuasua kwenye uzalishaji, Dk. Mwinyi alisema uwekezaji zaidi unahitajika ili yajiendeshe kibiashara na kusema serikali inahitaji uwekezaji mkubwa kwa baadhi yao ili kuwapa nafasi ya kufanya vizuri.

Akiyazungumzia mashirika ya umma yanayojiendesha yenyewe kama Shirika la Bima, ZMUX na mashirika mingine, Rais Dk. Mwinyi aliyashauri kutafuta mitaji na kujiendesha kibiashara hususan ZMUX ili kuendana na soko la ushindani.

Kuhusu Shirika la Nyumba Zanzibar, Dk. Mwinyi alilielezea shirika hilo kwamba halina kasi ya kujiendesha kwa kukosa mtaji wa kukarabati na kufanya matengenezo ya nyumba tangu zilipojengwa mwaka 1972 hadi sasa.

Pia Dk. Mwinyi alilishauri shirika hilo kuja na mpango utakaoonyesha mahitaji ya matengenezo na maboresho ya nyumba hizo ama kujenga mpya na kuonyesha marejesho ya uwekezaji ili nyumba hizo zileendelee kuleta tija kwa wananchi na Serikali. Pia alilitaka Shirika la Biashara Zanzibar (ZSTC) kubuni mbinu endelevu za uzalishaji kwa kuhakikisha wananunua karafuu zilizosafishwa ili kukwepa hasara kwa serikali.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SAUDA A JOKA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S1278/0085** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia MBEZI SECONDARY SCHOOL mwaka 2008. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DAR/URA/RB/78302/2023**


## PATA MKOPO KWA HARAKA

PATA MKOPO KWA HARAKA

**HADI 200,000,000/=**

KUTOKA

**ENTERPRISE FINANCE LIMITED**

KWAAJILI YA DHARURA

MBALIMBALI KAMA KULIPA

KODI YA NYUMBA,

KUNUNUA GARI,

KUBORESHA BIASHARA N.K

**TUNAPATIKANA**

DAR ES SALAAM **0677111333**

NA ARUSHA **0677226960.**

*1173303202*


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA,**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Bukoba**

**Kituo cha Bukoba Mjini Mkoa wa Kagera**

**Shauri la Madai Na. 84/2023**

**Jina la Mdai BADRU HUSSEIN KICHWABUTA**

**Jina la Mdaiwa FARUQ HUSSEIN ABDULREHMAN**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**

**Kwa FARUQ HUSSEIN ABDULREHMAN**

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao ya Tshs. 30,000,000 (milioni thelathini). Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 29 Mwezi 03 Mwaka 2023 saa 2:00 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati hii ya kuitwa shaurini, mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.
Hati hii imetolewa kwa amri na muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 07 Mwezi 03 Mwaka 2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO IRINGA YA BOMANI**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(MCA/84) R; 2002**

**SHAURI LA MADAI 12/2023.**

**MDAIWA: ....................SIFA SACCOS LTD**

**MDAIWA: .................SOPHIA KAWHILI**

**Mdaiwa: SOPHIA KAWHILI**

**Kwa ............ SOPHIA KAWHILI**

Shauri la madai tajwa hapo juu limefunguliwa katika Mahakama hii na SIFA SACCOS LTD, Mdaiwa popote pale unipo unaamriwa kufika kuhudhuria Mahakama tarehe 22/03/2023 saa 2:30asubuhi kujibu madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikiliza shauri hilo ni lazima kuleta mashaidi wako kwa ajili ya kujitetea bila kukosa. Usipofika bila taarifa shauri litasikilizwa upande mmoja na hukumu kutolewa.

Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 07/03/2023.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**
**WILAYA YA MOROGORO**
**KITUO CHA KINGOLWIRA**
**MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......3/2015**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: RAJABU A.KIBIKI WA MOROGORO**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA: NURU RAJABU KIBIKI**

**TANGAZO**

**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 16 Mwezi 3 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Endapo kuna yeyote mwenye Wosia wa Marehem anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 2 mwezi 3 mwaka 2023

## KUPOTEA KWA PASSPORT



**MICHAEL JOACHIM NGALO** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba **AB404561** iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 22/02/2016. Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe 21/02/2026. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **MBE/MBE/RB/74202/2023.**


**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com**

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0745 700 710.

Nipashe

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

# Poland kupeleka ndege vita Ukraine

**WARSAW, Poland**

RAIS wa Poland Andrzej Duda, alithibitisha nchi yake iko tayari kupeleka ndege yake aina ya MiG-29 kama msaada wa kivita kwa Ukraine.

Wakati kiongozi huyo anatoa kauli hiyo, vikosi vya Russia vinazidi kuishambulia nchi hiyo, na kuibua madai kwamba baadhi ya makombora yanalenga makazi ya watu.

Rais Duda alisema ndege hizo zilizobaki nchini Poland na ambazo sasa zinatumika katika jeshi la anga ziko tayari kuhamishwa hadi Ukraine.

"Nina hakika kwamba Ukraine itakuwa tayari kuzitumia mara moja," alisema Duda wakati akihojiwa na CNN.

Hapo awali alisema nchi yake ilifikiria kuhamisha ndege zake za Kisovieti hadi Ukraine.

Taarifa iliyotolewa na Wizara ya Ulinzi ya Poland, ilisisitiza kwamba Ukraine tayari ina marubani waliofundishwa kuzitumia vizuri.

Mapema Jumatano, Duda alitoa wito wa mafunzo kwa marubani wa Ukraine kutumia ndege za kivita za F-16, akisema kwamba katika siku zijazo, marubani wa nchi hiyo lazima wafikie viwango vya NATO.

Mchakato wa kutoa mafunzo kwa marubani kujua kuzitumia F-16 huchukua wastani wa mwaka mmoja.

Katika hatua nyingine, Russia imerusha makombora katika miji ya Kharkiv kaskazini , Odesa kusini na Zhytomyr.

Majengo ya makazi na miundombinu iliathiriwa pamoja na kukatiza huduma ya usambazaji umeme katika maeneo kadhaa.

Mashambulizi hayo yametokea huku mapigano makali ya ardhini yakiendelea katika mji wa Bakhmut mashariki mwa Ukraine.

Mkuu wa kijasusi wa Marekani alisema vita hivyo vitaendelea kwa miaka mingi.

Tangu vita hivyo vianze maelfu ya wapiganaji na raia wameuawa na kujeruhiwa, huku wengine wakikimbilia nchi jirani kwa ajili ya hifadhi.

Shambulizi kubwa la kombora lilipiga kituo cha nishati ya umeme katika mji wa bandari wa Odesa, na kusababisha kukatika kwa huduma hiyo.

Maeneo ya makazi pia yalikumbwa lakini hakuna majeruhi walioripotiwa.

"Takriban mashambulizi 15" yalipiga jiji la Odesa na eneo la Kharkiv, huku vifaa muhimu vya miundombinu na jengo la makazi likilengwa, mkuu wa utawala wa mkoa Oleg Synegubov alisema.

***BBC***




Polisi akirusha mabomu ya machozi kuwatawanya waandamanaji wanaoipinga serikali ya Sri Lanka wakati wa maandamano ya kutaka viongozi wa Shirikisho la Wanafunzi wa Vyuo Vikuu vya Inter waachiliwe. **PICHA: AFP**

# Watu 24 washtakiwa mahakamani kujihusisha mapenzi ya jinsia moja

**BUJUMBURA, Burundi**

WATU 24 nchini Burundi wamefikishwa mahakamani kwa makosa ya kujihusisha na mapenzi ya jinsia moja.

Serikali ya taifa hilo inaendesha msako dhidi ya watu wa jamii ya LGBTQ ambao kwa mujibu wa sheria ni kosa la jinai.

Februari 23 mwaka huu, Polisi iliwakamata wanaume 17 na wanawake saba waliokuwa kwenye warsha katika mji mkuu wa kisiasa wa Gitega, iliyondaliwa na shirika la hisani la MUCO Burundi, linaloangazia VVU na ugonjwa wa Ukimwi.

Armel Niyongere, ambaye ni mkuu wa kundi la haki za binadamu ACAT Burundi, alisema baada ya kuhojiwa kwa takriban siku 10, watu hao walishtakiwa na mwendesha mashtaka wa umma kwa kuhamasisha mapenzi ya jinsia moja. Pia wameshtakiwa kwa kosa la kujishughulisha na vitendo vya mapenzi ya jinsia moja vilivyoorodheshwa kama uhalifu unaobeba hukumu ya kifungo cha gerezani.

***DW***

# Kenya yashindwa kudhibiti uhaba wa dola

**NAIROBI, Kenya**

KENYA imetangaza kushindwa kudhibiti tatizo la uhaba wa pesa aina ya dola za Marekani, na kuibua wasiwasi wa kushuka kiuchumi.

Waziri wa biashara wa Kenya, Moses Kuria, alisema kuwa uhaba wa dola nchini humo umeshindwa kudhibitiwa na serikali.

Kuria aliwaambia wabunge juzi kwamba uhaba huo unaikabili dunia nzima lakini alilaumu utamaduni wa Wakenya wa kuagiza vitu nje ambavyo vinaweza kutengenezwa ndani ya nchi hiyo.

"Huwezi kuwa unalia kwamba tuna matatizo na dola wakati tunaagiza kila kitu nje ," alisema.

Alitoa wito wa kutolewa motisha ili kuwatia moyo wazalishaji wa bidhaa nchini humo na kuwalinda na washindani wa kigeni.

Benki kuu ya Kenya (CBK) imeyaagiza mabenki ya kibiashara kuwa na mgao wa zamu wa dola kufuatia uhaba wa sarafu hiyo, viliripoti vyombo vya habari nchini humo.

Wachambuzi wameilaumu CBK kwa mzozo wa kifedha, wakisema chombo hicho kilianzisha sheria kali katika soko la fedha kati ya mabenki na kuibua tatizo hilo.

Lakini benki hiyo imekuwa ikisema kuwa Kenya ina akiba ya kutosha ya fedha za kigeni kukidhi mahitaji.

Shilingi ya Kenya imepoteza thamani yake kwa asilimia 9 dhidi ya dola ya kimarekani katika kipindi cha mwaka mmoja, na hivyo kusababisha kupanda kwa gharama ya maisha.

***BBC***

## Nigeria yaahirisha uchaguzi wa gavana

**ABUJA, Nigeria**

TUME ya Uchaguzi nchini Nigeria imeahirisha uchaguzi wa magavana wa majimbo na mabaraza ya mitaa kwa muda wa wiki moja.

Upigaji kura ulitarajiwa kufanyika Jumamosi, lakini umesogezwa mbele hadi Machi 18 mwaka huu.

Vyama vya upinzani nchini humo vimetoa wito wa kuangaliwa kwa mashine za kielektroniki za kupiga kura, lakini mahakama ilikataa madai hayo.

Tume ya uchaguzi ilisema changamoto ya kisheria imechelewesha maandalizi na mashine hazitakuwa tayari kufanya kazi kwa wakati.

Ni jambo la kawaida kwa uchaguzi nchini humo kucheleweshwa , mnamo 2019, uchaguzi wa rais na bunge uliahirishwa kwa wiki moja.

Tume Huru ya Kitaifa ya Uchaguzi (INEC) ilianzisha Mfumo wa Ithibati ya Wapigakura wa Bimodal (BVAS) kwa mara ya kwanza kama sehemu ya teknolojia mpya iliyotumiwa katika uchaguzi wa mwaka huu katika jitihada za kuboresha uwazi.

Lakini makundi ya waangalizi na vyama vya upinzani vilisema ucheleweshaji mkubwa wa upigaji kura na kushindwa mfumo kufanya kazi wakati wa kutuma hesabu kuliruhusu kutokea kwa dosari wakati wa uchaguzi wa rais

***BBC***

**Ni jambo la kawaida kwa uchaguzi nchini humo kucheleweshwa , mnamo 2019, uchaguzi wa rais na bunge uliahirishwa kwa wiki moja.**

HABARI MICHEZO

# MINZIRO AKAMILISHA HESABU GEITA GOLD IKIWAVAA YANGA

**Na Shufaa Lyimo**

KIKOSI cha wachezaji 22 wa Geita Gold FC tayari kimewasili Dar es Salaam kwa ajili ya kujiandaa na mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Yanga utakaochezwa keshokutwa, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili jana kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Geita Gold, Fred Minziro, alisema kikosi chake kiko imara kuwakabili mabingwa hao watetezi licha ya kufanya vizuri kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya AS Real Bamako.

Minziro alisema wachezaji wake wote wako katika hali nzuri na wamejiandaa vyema huku akiamini watapata ushindi katika mchezo huo.

"Tumeingia mjini leo ( jana) alfajiri kwa ajili ya kujiandaa na mchezo huo, tunafahamu Yanga inashiriki mashindano ya kimataifa, hivyo tunapaswa kupambana kuhakikisha tunafanya vizuri," alisema Minziro. Aliongeza licha ya kuondokewa na wachezaji wengi msimu huu, bado hakuna kilichoharibika kwa sababu wanaendelea kuonyesha ushindani na wanajiimarisha zaidi kupitia programu mbalimbali wanazofanya mazoezini.

"Mazoezi tunayoendelea nayo ni ya kuwajenga wachezaji lakini pia tunawakumbusha wawe makini wakati wote wanapokuwa na wanapopoteza mpira," Minziro alisema.

Kocha huyo aliongeza Ligi Kuu Tanzania Bara ina ushindani mkubwa kutokana na kila timu kuhitaji kumaliza msimu ikiwa kwenye nafasi za juu.

"Makosa ya kiufundi niliyoyabaini katika michezo iliyopita nimeyafanyia kazi, ninaamini hayatajitokeza kwa mara nyingine, ingawa wachezaji wangu wengi wameondoka katika msimu huu, bado tunaendelea kupambana, kila mmoja ameona uwezo wa kikosi changu, ninawaomba mashabiki wetu waendeleze ushirikiano ili tutimize malengo yetu," Minziro alisema.

Hata hivyo anaendelea kuwashukuru wachezaji wake kwa kufuata maelekezo anayowapa nje na ndani ya uwanja ambayo yanasaidia kupata matokeo mazuri kila wanaposhuka dimbani na hawapotezi mechi kirahisi.




Wajumbe wa Chama cha Mpira wa Miguu cha Mkoa wa Simiyu (SIFA), wakiwa katika picha ya pamoja baada ya kumaliza mkutano mkuu wa kawaida wa chama hicho uliofanyika Jumapili iliyopita mkoani humo. **PICHA: MTANDAO**

# JKT TZ yanusa Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya JKT Tanzania imeendelea kutoa vichapo katika Ligi ya Championship baada ya kuifunga Ndanda FC mabao 4-1 katika mechi ya ligi hiyo iliyochezwa kwenye Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Dar es Salaam juzi na kuanza kunusa harufu ya kucheza Ligi Kuu Bara msimu ujao.

Mabao ya JKT Tanzania katika mechi hiyo yaliwekwa katika kamba na Edward Songo aliyepachika mawili, Elia Ashley na Himid Selemani.

Ushindi huo umewafanya JKT Tanzania kufikisha pointi 50 baada ya kucheza mechi 20, wakishinda michezo 16, sare mbili na kupoteza mechi mbili.

Ndiyo timu yenye uhakika mkubwa wa kupanda daraja moja kwa moja na kucheza Ligi Kuu Tanzania Bara katika msimu mpya wa mwaka 2023/24, Ligi ya Championship imebakisha raundi tisa ili kumalizika.

JKT Tanzania ilishuka daraja msimu wa 2020/21 pamoja na Ihefu ambayo ilirejea Ligi Kuu msimu huu, Gwambina FC na Mwadui.

Kitayosce ya Tabora inashika nafasi ya pili katika msimamo wa ligi hiyo ikiwa na pointi 42 ikifuatiwa na Pamba ya Mwanza yenye pointi 38.

## Ruvu Shooting yatangaza vita

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI leo inashuka ugenini kuwakabili Mbeya City katika mechi ya Ligi Kuu Bara itakayochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini, Mbeya, Ruvu Shooting imetangaza hali ya hatari katika mechi zake sita zilizobakia.

Msemaji wa Ruvu Shooting, Masau Bwire, alisema mechi hizo ni za ukombozi kwa timu yao inayoburuza mkia na ahadi ya kupata matokeo chanya wanaianza leo watakapowavaa Mbeya City.

"Kikosi kiko jijini Mbeya muda mrefu, kiko huko kwa shughuli maalum ya kuhakikisha hizi mechi tulizosalia nazo zinaleta ukombozi kwenye klabu yetu, kwa hiyo ni lazima tujidhatiti, tujiweke vizuri ili tukae eneo salama, tuliwahi kwa lengo la kusoma mazingira yasije yakawaathiri vijana watapokuwa uwanjani wakiitetea timu yao," alisema Bwire.

Alisema wameandaa mpango maalum wa kiufundi wa kuhakikisha timu hiyo haishuki daraja kwa kuimarisha umoja kuanzia kwa wachezaji, benchi la ufundi na viongozi wa timu hiyo.

Ruvu Shooting yenye pointi saba imecheza mechi 24 na kati ya hizo imeshinda michezo minne, sare tano na kupoteza

## Wanariadha Afrika Mashariki kuchuana

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya riadha ya vijana wa umri chini ya miaka 18 na 20 ya Afrika Mashariki na Kati yanatarajiwa kufanyika leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa Shirikisho la Riadha Tanzania (RT), Lwiza John, alisema washiriki 232 wamethibitisha kushiriki mashindano hayo yatakayofanyika kwa siku mbili.

Lwiza alizitaja nchi zitakazoleta washiriki wa mashindano hayo ni pamoja na Eritrea, Somalia, Ethiopia, Zanzibar, Sudan, Sudan Kusini, Uganda, Kenya na Tanzania.

"Kila nchi inatakiwa kuleta wanariadha 20, wanawake 10 na wanaume 10, maandalizi yanaendelea vizuri kuhakikisha michuano hii inafanyika kwa weledi na washindi wanapatikana," alisema Lwiza.

Alitoa wito kwa mashabiki na wapenzi wa riadha kujitokeza kwa wingi kushangilia kwa lengo la kuongeza molari kwa vijana wanaoshiriki mashindano hayo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### UNITED YAMTAKA CAMAVINGA

MANCHESTER United iko tayari kutoa euro milioni 130 kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Eduardo Camavinga, mwenye umri wa miaka 20 kutoka Real Madrid. ***(Fichajes)***

### TEN HAG AMTAKA KANE, KUDUS

MSHAMBULIAJI wa Tottenham Hotspur na England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 29, yuko kwenye orodha ya usajili ya Kocha wa Manchester United, Erik ten Hag, kama ilivyo kwa kiungo mshambuliaji wa Ghana, Mohammed Kudus (22), kutoka klabu ya zamani ya Mholanzi huyo ya Ajax. ***(TalkSport)***

### BEI YA JUDE HAIPUNGUI

KLABU ya Borussia Dortmund haitaondoa thamani yao ya euro milioni 150 ya kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya England, Jude Bellingham, mwenye umri wa miaka 19 huku Liverpool, Manchester City na Real Madrid zikionyesha nia ya kumtaka. ***(90 min)***

### LIVERPOOL YAZIDI KUJIPANGA

LIVERPOOL inazidi kujiamini itashinda mbio za kuinasa saini ya Jude Bellingham, lakini matumaini yao ya kufanya hivyo huenda yakaegemea kwenye jitihada zao za kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(Mail)***

### BOTMAN ANUKIA NEWCASTLE

KLABU ya Paris St-Germain imeonyesha nia ya kumsajili beki wa Newcastle United, Mholanzi Sven Botman mwenye umri wa miaka 23. ***(iNews)***

### KOCH AGEUKA LULU

MLINZI wa Leeds United, Robin Koch, mwenye umri wa miaka 26 anazingatiwa kama mchezaji anayetarajiwa kusajiliwa na Newcastle United, ingawa klabu kadhaa za Ligi Kuu Ujerumani, pia zinavutiwa naye. ***(Sport1)***

### HAZARD KUBAKIA MADRID

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Eden Hazard mwenye umri wa miaka 32, anapanga kubakia Real Madrid hadi mkataba wake utakapokamilika hapo mwakani. ***(Athletic)***

### CANCELO ATAKIWA JUMLA

KLABU ya Bayern Munich itakataa nafasi ya kufanya usajili wa mkopo wa beki wa pembeni wa Manchester City, Joao Cancelo, mwenye umri wa miaka 28 kuwa wa kudumu kwa pauni milioni 62. ***( Calciomercato, Via Mail)***

### RAPHINHA HUYO NEWCASTLE

NEWCASTLE United inaweza kuwashawishi Barcelona kumuuza winga wa Brazil, Raphinha, mwenye umri wa miaka 26, ikiwa wanaweza kufikia ada ya pauni milioni 55 ambayo klabu hiyo ya Hispania ililipa kumsajili kutoka Leeds United mwaka jana. ***(El Desmarque)***

### MOUNT ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL inaongoza katika kinyang'anyiro cha kumsajili mchezaji wa kimataifa wa England, Mason Mount, mwenye umri wa miaka 24 kutoka Chelsea na Mreno Matheus Nunes (24) kutoka Wolves, huku Kocha Jurgen Klopp akijaribu kurekebisha safu yake ya mashambulizi. ***(Mail)***

### MARTINEZ AGOMBEWA ULAYA

KLABU ya Aston Villa inataka kumsajili mlinzi wa Athletic Bilbao, Inigo Martinez, kwa uhamisho wa bila malipo msimu wa joto, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Barcelona na Atletico Madrid ili kumnunua mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31 ambaye hana mkataba. ***(Mail in Birmingham)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# MBAPPE: NAFIKIRIA UBINGWA LIGUE 1 TU

●●●Mshambuliaji huyo afunguka baada ya PSG kuondolewa katika...

**PARIS, Ufaransa**

KYLIAN Mbappe amesisitiza kuondolewa kwa Paris Saint-Germain kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Bayern Munich hakutaathiri mustakabali wake kwa sababu kwa sasa mshambuliaji huyo anauangalia ubingwa wa Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

Mabao ya Eric Maxim Choupo-Moting na Serge Gnabry kipindi cha pili kwenye Uwanja wa Allianz Arena Jumatano, yaliwahakikishia Bayern Munich ushindi wa mabao 2-0 na ushindi wa uwiano wa magoli 3-0 katika mchezo huo wa pili wa hatua ya 16 bora.

Hii ilikuwa mara ya pili mfululizo kwa PSG kuondolewa katika hatua hiyo kwenye mashindano hayo, ambayo mara kadhaa wamelazimika kupambana na Real Madrid ili kumbakisha Mbappe katika mji mkuu wa Ufaransa.

Mbappe, mchezaji wa kimataifa wa Ufaransa hapo awali alikanusha mapendekezo ya kuwa taji la Ulaya ndilo litakaloamua mustakabali wake.

Alipoulizwa na waandishi wa habari iwapo kuondolewa kutaathiri mustakabali wake, Mbappe alijibu: "Hapana, hapana, nimetulia, jambo pekee ambalo ni muhimu kwangu msimu huu ni kutwaa ubingwa wa ligi, halafu tutaona."

Vijana hao wa Kocha Christophe Galtier, wako mbele kwa pointi nane kileleni mwa msimamo wa Ligue 1 wakilenga kutetea taji lao.

Hata hivyo, Kocha Mauricio Pochettino, alifukuzwa msimu uliopita kwa kushindwa katika raundi hiyo hiyo ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, ambapo walipoteza mchezo dhidi ya walioibuka mabingwa Real Madrid chini ya Kocha Carlo Ancelotti.

PSG wamecheza mechi 137 katika mashindano ya UEFA ya klabu za juu bila kunyanyua kombe, ni Arsenal tu (177) ndio wanaoongoza kwa kucheza mechi nyingi za mashindano hayo bila kutwaa taji.

Vijana wa Galtier walikuwa na bahati mbaya mjini Munich, wakati Vitinha alipofanya uzembe na kusababisha bao la wazi lililowekwa kimiani na Matthijs de Ligt.

Mbappe alikubali kulikuwa na machache ya kutenganisha pande hizo mbili za ubora wa juu, ingawa hiyo haikusaidia sana kumaliza kuchanganyikiwa kwake.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24 aliongeza: "Tumekata tamaa. Ndivyo ilivyo, tunapaswa kusonga mbele, kujaribu kutoa changamoto kwa kila mtu.

"Hatukukosa sana tulipoangalia hali ya timu hizo mbili, lakini wana timu iliyojengwa kushinda Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Mwanzoni mwa msimu, wakati wa mkutano wa kwanza na waandishi wa habari wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, nilisema tutafanya kila tuwezalo na kutoa uwezo wetu.

"Tutajihoji na kurudi kwenye maisha yetu ya kila siku kwenye Ligue 1."

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,087,3

MECHI KALI
MBEYA CITY
VERSUS
RUVU SHOOTING
1 | 2.07
X | 2.90
2 | 3.54

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MESSI AVUTWA LIGI KUU MAREKANI




**MIAMI, Marekani**

LIONEL Messi kuhamia kwenye Ligi Kuu ya Marekani, MLS, na kujiunga na Inter Miami utakuwa “usajili mkubwa zaidi katika historia”, kwa mujibu wa kocha mkuu wa klabu hiyo, Phil Neville.

Mshindi huyo mara saba wa tuzo ya Ballon d’Or amekuwa akihusishwa sana na kuhamia Marekani na yuko ndani ya miezi sita ya mwisho ya mkataba wake na Paris Saint-Germain.

Vigogo wa Ligue 1, PSG wana nia ya kuhifadhi huduma za mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35, ambaye aliongoza Kombe la Dunia katika mataji yake mwaka jana.

Kuhamia MLS kutamfanya Messi kufuata nyayo za mmiliki mwenza wa Miami, David Beckham, Andrea Pirlo na Steven Gerrard.

Neville anaamini huo utakuwa usajili mkubwa zaidi, na akasisitiza Messi ni aina ya mchezaji ambaye klabu yake inamhitaji kwa sasa.

“Nadhani labda huu atakuwa usajili mkubwa zaidi katika historia,” alisema akiambia Athletic.

“Siwezi kufikiria juu ya nyota mwingine wa kiwango hicho kuja kutoka nchi kubwa ya soka mahali hapa. Hii labda ni sawa na kuwasili kwa Beckham, lakini labda kubwa zaidi.

# Conte akataa kujiuzulu Spurs

**LONDON, England**

ANTONIO Conte amesema anafuraha kubaki kama kocha wa Tottenham Hotspur licha ya timu yake kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na AC Milan, hapo juzi.

Spurs ililala kwa jumla ya uwiano wa bao 1-0 (wakiwa wamepoteza mchezo wa kwanza 1-0), baada ya sare kwenye mchezo wa pili Kaskazini mwa London juzi, huku mashabiki wa nyumbani wakionyesha hasira zao dhidi ya kocha huyo wa Italia katika kipenga cha mwisho.

Wakiwa wametoka pia katika Kombe la FA dhidi ya Sheffield United wiki moja iliyopita, msimu wa 2022-23 utakuwa usio na taji kwa Spurs na nafasi yao ya nne bora kwenye Ligi Kuu England ipo kwenye tishio kubwa.



Kumekuwa na uvumi unaoongezeka juu ya mustakabali wa kocha huyo mwenye umri wa miaka 53, lakini katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, hakuonesha dalili za kuondoka hivi karibuni.

Conte alisema: “Hii sio siku sahihi kuzungumzia mustakabali wangu, lakini nina mkataba na Tottenham.

“Tottenham wanafahamu vyema mawazo yangu, mwisho wa msimu tutakutana kisha tutafanya uamuzi.

“Nadhani hali iko wazi. Mwaka mmoja na miezi mitatu tangu nianze kuwa kocha wa Tottenham na huwa nasema kitu kimoja - tunahitaji kuwa na muda na subira.

## HABARI MICHEZO

305,640/-

# MANDONGA SASA KUITAMBULISHA MLUNGAMBUNGA ULINGONI KENYA

**Na Mwandishi Wetu**

BONDIA maarufu nchini, Karim Mandonga, ametangaza 'kiama' kwa mpinzani wake, Mganda Keneth Lukyamuzi katika pambano litakalofanyika Machi 25, mwaka huu kwenye Ukumbi wa KICC jijini Nairobi, Kenya.

Akizungumza katika makao makuu ya DStv Tanzania, Mandonga, alisema pambano hilo la kukata na shoka ambalo litarushwa mubashara ndani ya DStv, litakuwa la kukata ngebe za mpinzani wake na mabondia wengine wote wa Afrika Mashariki kwa sababu safari hii ana ngumi mahsusi inayojulikana kwa jina la 'Mlungambunga'

"Waafrika wote wajiandae kushuhudia mtu akisulubiwa ulingoni siku hiyo mubashara ndani ya DStv," alisema Mandonga na kusisitiza atamchapa mpinzani wake mapema sana kwa 'knock out'.

"Nimefurahi sana kwa DStv kukubali kuonyesha pambano hili kwani hii italifanya lionekane kote Afrika. Huu ni wakati wa kuionyesha Afrika na dunia kuwa Mandonga ni mtu kazi kweli kweli. Naenda kutuma salamu. Kama kuna bondia yeyote anayejiamini aje mimi kazi yangu ni moja tu - kumchapa," alijigamba Mandonga.

Naye Mkuu wa Masoko wa MultiChoice Tanzania, Ronald Shelukindo, alisema ili kuhakikisha Watanzania wengi wanashuhudia pambano hilo, DStv italionyesha mubashara kupitia chaneli ya Maisha Magic Bongo inayopatikana katika kifurushi cha DStv Bomba kwa gharama ya Sh. 23,000.

Itakumbukwa kuwa hivi karibuni bondia Mandonga alipata umaarufu mkubwa sana Kenya baada ya kumtwanga Mkenya, William Wanyonyi.

Mapambano ya utangulizi yatakayofanyika siku hiyo yatakuwa ni kati ya Nik Otieno dhidi ya Hassan Ndongo, George Bonabucha vs Michael Diares, Consolata Musanga vs Fatuma Yazidu na Zawadi Kutaka atapambana na Plaxedus Odwor.




Bondia Karim Mangonda (katikati) akitangaza rasmi anatarajia kupanda ulingoni kuchuana na Keneth Lukyamuzi kutoka Uganda katika pambano litakalofanyika Machi 25, mwaka huu kwenye Ukumbi wa KICC jijini Nairobi, Kenya. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Nabi afichua siri

INATOKA UK. 24

Said, amefurahishwa na ushindi huo waliopata na kusema wanahitaji kumaliza kazi katika mchezo wao unaofuata.



"Ninawapongeza wachezaji wetu kwa kazi kubwa waliyoifanya leo (juzi), tuna matumaini makubwa ya kuingia hatua ya robo fainali ya mashindano haya, tunataka kutimiza malengo yetu ya muda mrefu," alisema Hersi.

Rais huyo alisema mafanikio hayo yametokana na ushirikiano na umoja walionao kuanzia kwa viongozi, benchi la ufundi na viongozi wa klabu na kuwaahidi mashabiki wao wataendeleza mambo mazuri.

Nyota wa zamani wa timu hiyo, Sunday Manara, alisema Yanga ilicheza vizuri na kuongeza kwa sasa wana kikosi imara chenye uwezo mkubwa wa kuwapa mashabiki furaha.

"Nimeridhishwa na kiwango kizuri kilichoonyeshwa na kikosi chetu ambacho kila mchezaji alifanya kile alichoagizwa na benchi la ufundi, nasema wachezaji walijitahidi kutawala mpira kwa kiasi kikubwa," Manara alisema.

# Simba kuifanya Mtibwa daraja

INATOKA UK. 24

hitaji pointi tatu ili kujihakikisha kufuzu kucheza robo fainali, tukiungana kwa pamoja tunafanikiwa malengo yetu," alisema Ahmed.

Katika mechi ya kesho, Simba itawakosa nyota wake wanne ambao ni Kibu Denis, Ismael Sawadogo na Augustine Okrah ambao ni majeruhi na kipa chaguo la pili, Beno Kakolanya, ambaye ana ruhusa maalum kwa ajili ya kumaliza matatizo yake ya kifamilia.


SUPA JACKPOT

MECHI WIKI HII

BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/03/23 | 18:00 | Everton FC vs Brentford FC | 2.55 | 3.05 | 2.70 |
| 02. 11/03/23 | 18:00 | Preston North End vs Cardiff City | 2.55 | 3.10 | 2.70 |
| 03. 11/03/23 | 18:00 | Queens Park Rangers vs Watford FC | 2.65 | 3.15 | 2.50 |
| 04. 11/03/23 | 18:15 | Elche CF vs Real Valladolid | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 05. 11/03/23 | 18:30 | FC Pacos Ferreira vs Santa Clara Azores | 2.31 | 3.15 | 2.95 |
| 06. 11/03/23 | 20:15 | KAS Eupen vs KV Oostende | 2.46 | 3.30 | 2.60 |
| 07. 11/03/23 | 22:45 | Bologna FC vs Lazio Rome | 2.95 | 3.15 | 2.29 |
| 08. 11/03/23 | 23:00 | Sparta Rotterdam vs Vitesse Arnhem | 2.35 | 3.25 | 2.80 |
| 09. 12/03/23 | 14:15 | NEC Nijmegen vs FC Utrecht | 2.45 | 3.20 | 2.70 |
| 10 12/03/23 | 14:30 | US Lecce vs Torino FC | 2.85 | 2.90 | 2.55 |
| 11. 12/03/23 | 16:00 | RCD Mallorca vs Real Sociedad San Sebastian | 3.20 | 2.85 | 2.36 |
| 12. 12/03/23 | 17:00 | AC Ajaccio vs Montpellier HSC | 2.75 | 3.10 | 2.50 |
| 13. 12/03/23 | 17:00 | FC Nantes vs OGC Nice | 3.05 | 3.10 | 2.28 |
| 14. 12/03/23 | 17:00 | Hellas Verona vs AC Monza | 2.36 | 3.05 | 2.95 |
| 15. 12/03/23 | 18:30 | Rio Ave FC vs Gil Vicente Barcelos | 2.28 | 3.10 | 3.05 |
| 16. 12/03/23 | 20:30 | KRC Genk vs Union Saint-Gilloise | 2.29 | 3.40 | 3.05 |
| 17. 12/03/23 | 21:30 | VfL Wolfsburg vs Union Berlin | 2.26 | 3.20 | 3.30 |

MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

IJUMAA - 10/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1782 | Perth Glory vs Western Sydney | 2.89 | 3.25 | 2.32 |
| 16:00 | 4002 | Mbeya City vs Ruvu Shooting | 2.07 | 2.90 | 3.54 |
| 16:00 | 5806 | Maccabi Jaffa vs Ironi Hasharon | 2.19 | 3.13 | 3.29 |
| 16:45 | 2192 | AL Bataeh (UAE) vs Al Dhafra | 2.05 | 3.38 | 3.07 |
| 16:45 | 5633 | AL Khaleej Khor Fakkan vs Ajman Club | 2.40 | 3.23 | 2.61 |
| 17:00 | 1695 | AL Qadsia vs AL Arabi | 2.39 | 3.14 | 2.68 |
| 17:00 | 2431 | MC Magra vs MC Alger | 2.51 | 2.80 | 2.90 |
| 17:00 | 3368 | El Bayadh vs US Biskra | 1.73 | 2.97 | 5.42 |
| 17:00 | 3868 | RC Arbaa vs JS Saoura | 2.65 | 2.91 | 2.65 |
| 18:30 | 5226 | Botosani vs CS Mioveni | 1.97 | 3.19 | 3.72 |
| 19:00 | 2256 | HNK Gorica vs Istra | 2.38 | 3.03 | 2.77 |
| 19:00 | 2596 | Sochi vs Gazovik Orenburg | 1.81 | 3.67 | 3.77 |
| 19:00 | 5849 | Pribram vs SK Lisen | 2.31 | 3.15 | 2.78 |
| 19:30 | 1211 | ND Gorica vs NK Mura | 3.28 | 3.33 | 1.98 |
| 19:30 | 1445 | AL Wahda Scc (UAE) vs Al Ain | 2.78 | 3.25 | 2.26 |
| 19:30 | 1447 | Dibba Al Fujairah vs Ittihad Kalba | 3.35 | 3.40 | 1.94 |
| 19:30 | 2959 | AS Trencin vs Ruzomberok | 2.18 | 3.24 | 2.93 |
| 20:00 | 2094 | Lechia Gdansk vs Miedz Legnica | 2.39 | 3.17 | 2.66 |
| 20:00 | 2982 | Giresunspor vs Fatih Karagumruk | 2.43 | 3.32 | 2.69 |
| 20:30 | 2027 | Nurnberg vs Eintracht Braunschweig | 2.05 | 3.43 | 3.33 |
| 20:30 | 5309 | Kaiserslautern vs Sandhausen | 1.74 | 3.63 | 4.33 |
| 21:00 | 4018 | Odense vs Aalborg | 2.21 | 3.40 | 3.04 |
| 21:00 | 4351 | Moreirense vs Penafiel | 1.84 | 3.53 | 3.74 |
| 21:30 | 1934 | Chateauroux vs Concarneau | 2.57 | 3.10 | 2.68 |
| 21:30 | 3386 | Avranches vs Le Mans | 3.05 | 3.20 | 2.25 |
| 21:30 | 3486 | Universitatea Craiova vs UTA Arad | 1.73 | 3.45 | 4.49 |
| 22:00 | 1116 | FC Oss vs ADO Den Haag | 3.23 | 3.29 | 2.08 |
| 22:00 | 1643 | FC Eindhoven vs Jong Ajax | 1.89 | 3.53 | 3.53 |
| 22:00 | 2096 | Almere City vs Jong Utrecht | 1.44 | 4.27 | 6.04 |
| 22:00 | 2149 | GO Ahead Eagles vs Waalwick | 2.07 | 3.40 | 3.20 |
| 22:00 | 2283 | VVV Venlo vs Den Bosch | 1.55 | 4.01 | 4.99 |
| 22:00 | 2634 | Dordrecht vs De Graafschap | 3.80 | 3.49 | 1.83 |
| 22:00 | 2842 | Helmond Sport vs Jong PSV | 2.34 | 3.21 | 2.80 |
| 22:00 | 4593 | Willem II Tilburg vs PEC Zwolle | 2.56 | 3.23 | 2.53 |
| 22:00 | 5538 | Heracles Almelo vs Jong AZ Alkmaar | 1.38 | 4.80 | 6.26 |
| 22:00 | 5770 | Roda Kerkrade vs Telstar | 2.01 | 3.32 | 3.37 |
| 22:00 | 5986 | NAC Breda vs Maastricht | 1.70 | 3.85 | 4.06 |
| 22:15 | 1251 | FC Schaffhausen vs Lausanne-Sport | 3.56 | 3.45 | 1.85 |
| 22:30 | 2425 | FC Koln vs VfL Bochum | 1.60 | 3.81 | 4.91 |
| 22:30 | 2645 | Cagliari vs Ascoli | 2.07 | 3.14 | 3.46 |
| 22:45 | 1988 | Crewe vs Salford City | 3.56 | 3.36 | 1.92 |
| 22:45 | 2517 | Inverness vs Kilmarnock | 3.30 | 3.36 | 2.00 |
| 22:45 | 3054 | Charleroi vs OH Leuven | 2.01 | 3.46 | 3.36 |
| 22:45 | 4765 | St Patricks vs Bohemians FC | 2.14 | 3.14 | 3.09 |
| 22:45 | 5789 | Spezia vs Inter | 6.59 | 4.39 | 1.41 |
| 23:00 | 1928 | Real Oviedo vs Tenerife | 2.66 | 2.71 | 2.91 |
| 23:00 | 1976 | Lille vs Lyon | 1.90 | 3.55 | 3.55 |
| 23:00 | 4456 | Cadiz CF vs Getafe | 2.42 | 2.79 | 3.14 |
| 23:00 | 4752 | Stoke City vs Blackburn | 2.01 | 3.35 | 3.40 |
| 23:15 | 5772 | Porto vs GD Estoril | 1.20 | 5.82 | 12.05 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# Michezo

Ijumaa Machi 10, 2023
Nipashe



UKURASA 21

## Mbappe: Nafikiria ubingwa Ligue 1 tu




Kiungo wa Yanga, Mudathir Yahya (katikati), akijiandaa kuwatoka wachezaji wa AS Real De Bamako kutoka Mali katika mechi ya mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi usiku. Yanga ilishinda mabao 2-0. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NABI AFICHUA SIRI YA USHINDI YANGA

●●●Aeleza bado hawajamaliza kazi, Hersi amwaga pongezi kwa...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kupata ushindi na kufikisha pointi saba, Kocha Mkuu wa Yanga ambaye ni raia wa Tunisia, Nasreddine Nabi, amesema kikosi chake kilivuna matokeo chanya kutokana na wachezaji kujituma na kucheza katika kiwango cha juu.

Ushindi wa mabao 2-0 walioupata Yanga dhidi ya AS Real De Bamako kutoka Mali uliwafanya mabingwa hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara kung'ang'ania katika nafasi ya pili kwenye Kundi C katika michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Vinara wa kundi hilo ni US Monastir ya Tunisia yenye pointi 10 wakati TP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) yenye pointi tatu iko katika nafasi ya tatu na AS Real De Bamako inaburuza mkia ikiwa na pointi mbili.

Nabi alisema ushindi walioupata umesababishwa na wachezaji wake kufuata vyema maelekezo yanayotolewa na benchi la ufundi la timu hiyo.

Kocha huyo aliwapongeza wachezaji wa timu hiyo kwa kupambana na kurejesha matumaini ya kusonga mbele kwa sababu mchezo huo ulikuwa mguu na wapinzani wao Real Bamako walionyesha ushindani wakati wote.

"Nawapongeza wachezaji wangu kwa kucheza vizuri hasa katika kipindi cha pili, ninaamini tulikuwa bora katika matukio mengi ukilinganisha na wapinzani wetu, hii ni ishara njema kuelekea mchezo wetu unaokuja dhidi ya US Monastir," alisema Nabi.

Aliongeza aliamua kumtoa Stephen Aziz Ki kwa sababu nyota huyo alishindwa kutekeleza vyema majukumu yake katika kipindi cha kwanza hali iliyosababisha wapinzani wao watawale kwenye eneo la kiungo.

Mtunisia huyo alisema ni hali ya kawaida kufanya mabadiliko ya wachezaji ingawa amepanga kuzungumza naye kwa lengo kumrejesha katika kiwango chake kwa faida ya timu.

"Hakuna anayepinga Aziz Ki ni mchezaji bora kutokana na uwezo wake lakini leo (juzi) hakutimiza ipasavyo majukumu yake, ni jambo la kawaida lakini, hakuwa peke yake ila kama kocha nitazungumza naye kwa upendo ili kuepukana na tatizo hilo," alisema Nabi.

Naye Kocha Mkuu wa AS Real De Bamako, Nouhoum Diane, alisema alifahamu mechi hiyo itakuwa ngumu kwao kutokana na ubora waliokuwa nao Yanga iliyocheza mbele ya mashabiki wake wa nyumbani.

Diane alisema timu yake ilikutana na wakati mgumu wa kupambana na Yanga yenye wachezaji wenye uzoefu mkubwa katika mashindano ya kimataifa, safu nzuri ya ushambuliaji na pia ina nguvu ya fedha.

"Nawapongeza Yanga na tunakubali matokeo, lakini pamoja na kupoteza mchezo hatukuwa wepesi, wenyewe mmeshuhudia mchezo ulivyokuwa mgumu na wenye ushindani, tuliushika mchezo katika baadhi ya nyakati lakini wenyeji walikuwa bora dhidi yetu," alisema Diane.

Wakati huo huo, Rais wa Yanga, Hersi

INAENDELEA UK. 23

## Simba kuifanya Mtibwa daraja

**Na Saada Akida**

IKIWA imefika salama mkoani Morogoro, Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera 'Robertinho', amesema anatarajia kutumia Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa kesho kama sehemu ya maandalizi ya kuwakabili Horoya AC kutoka Guinea.

Simba itaikaribisha Horoya AC katika mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa Machi 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Robertinho aliliambia gazeti hili kikosi chake kiko imara na tayari kuzisaka pointi tatu dhidi ya Mtibwa Sugar ili kuendelea kujiweka katika sehemu salama kwenye mbio zao za kuwania ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kocha huyo alisema anafahamu Mtibwa Sugar ni moja ya timu nzuri hapa nchini, hivyo watacheza kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha wanaendelea kujiimarisha kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Kupata pointi tatu kutoka kwa Mtibwa Sugar kutatupa morali kuelekea mechi ijayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Horoya AC. Tunataka kuendelea kupata matokeo bora, itatusaidia kujiamini zaidi," alisema kocha huyo.

Aliongeza mechi hiyo dhidi ya Mtibwa Sugar itakuwa na ushindani kwa sababu wenyeji wanahitaji kulinda heshima ya kucheza nyumbani na wao wanahitaji kuondoka na pointi tatu muhimu.

"Tunaifahamu Mtibwa Sugar, tunajua haitakuwa mechi rahisi kutokana na ubora walionao hasa kwa sababu watakuwa wanacheza kwenye Uwanja wa nyumbani, tunahitaji matokeo chanya katika mchezo wetu wa Jumamosi.

Hii mechi itakuwa na mambo mawili, kuhitaji ushindi na kurejea nyumbani na pointi moja, lakini inawapa wachezaji wangu molari kuelekea mechi yetu ijayo ya kimataifa," alisema Kocha huyo.

Naye Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano Simba, Ahmed Ally, alisema kikosi kipo vizuri kuelekea mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar na wanatambua umuhimu wa mchezo huo.

"Niwaomba mashabiki wa Simba baada ya mechi yetu ya ligi, waanze maandalizi ya mchezo wetu wa mwisho wa nyumbani wa Ligi ya Mabingwa Afrika. Mechi hiyo ni muhimu sana kwa sababu tuna-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >